القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation


by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy
(Former Chief Kadhi of
Zanzibar & Kenya)

88. Wakuu waliotakabari katika kaumu yake wakasema: "Ewe Shuebu! Tutakutoa wewe na wale walioamini pamoja nawe katika mji wetu, au mrejee katika mila yetu." Akasema: "Je, ingawa tunaichukia?"

قَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ اسْتَكْبَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَنُخْرِجَنَّكَ
يَا شُعَيْبُ وَالَّذِينَ آمَنُوا مَعَكَ مِنْ قَرْيَتِنَا أَوْ
لَتَعُودُنَّ فِي مِلَّتِنَا ۚ قَالَ أَوَلَوْ كُنَّا كَارِهِينَ ﴿٨٨﴾

89. "Bila shaka tumemtungia Mwenyezi Mungu uwongo ikiwa tutarudi katika mila yenu baada ya Mwenyezi Mungu kutuokoa nayo. Wala haiwi kwetu sisi kurejea mila hiyo. Lakini akitaka (jambo) Mwenyezi Mungu, Mola wetu, (huwa). Mola wetu amekienea kila kitu kwa ilimu yake. Kwa Mwenyezi Mungu tunategemea. Mola wetu! Hukumu baina yetu na baina ya wenzetu (hawa) kwa haki, nawe ndiye mbora wa wanaohukumu."

قَدِ افْتَرَيْنَا عَلَى اللَّهِ كَذِبًا إِنْ عُدْنَا فِي مِلَّتِكُمْ
بَعْدَ إِذْ نَجَّانَا اللَّهُ مِنْهَا ۚ وَمَا يَكُونُ لَنَا أَنْ نَعُودَ
فِيهَا إِلَّا أَنْ يَشَاءَ اللَّهُ رَبُّنَا ۚ وَسِعَ رَبُّنَا كُلَّ
شَيْءٍ عِلْمًا ۚ عَلَى اللَّهِ تَوَكَّلْنَا ۚ رَبَّنَا افْتَحْ بَيْنَنَا وَ
بَيْنَ قَوْمِنَا بِالْحَقِّ وَأَنْتَ خَيْرُ الْفَاتِحِينَ ﴿٨٩﴾

90. Na wakuu waliokufuru katika kaumu yake wakasema: "Kama nyinyi mkimfuata Shuebu, hapo bila shaka mtakuwa wenye kukhasirika."

وَقَالَ الْمَلَأُ الَّذِينَ كَفَرُوا مِنْ قَوْمِهِ لَئِنِ اتَّبَعْتُمْ شُعَيْبًا
إِنَّكُمْ إِذًا لَخَاسِرُونَ ﴿٩٠﴾

91. Basi mtetemeko wa ardhi uliwatoa roho zao, wakawa wasiojimudu, (wamekufa) humo mjini mwao.

فَأَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ فَأَصْبَحُوا فِي دَارِهِمْ
جَاثِمِينَ ﴿٩١﴾

92. Wale waliomkadhibisha Shuebu wakawa kama kwamba hawakuwako (mahala hapo). Wale waliomkadhibisha Shuebu ndio waliokuwa wenye khasara.

الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَأَنْ لَمْ يَغْنَوْا فِيهَا ۚ
الَّذِينَ كَذَّبُوا شُعَيْبًا كَانُوا هُمُ الْخَاسِرِينَ ﴿٩٢﴾

93. Basi (ulipoadia wakati wa kuangamizwa wabaya hao, Nabii Shuebu alitoka nchi ile pamoja na wale waliomuamini) akawaachilia mbali (akenda zake) na akasema: "Enyi kaumu yangu! Nimekufikishieni ujumbe wa Mola wangu na nimekupeni nasaha; basi nihuzunikeje juu (yenu, nyinyi) watu makafiri?"

فَتَوَلَّىٰ عَنْهُمْ وَقَالَ يَا قَوْمِ لَقَدْ أَبْلَغْتُكُمْ رِسَالَاتِ
رَبِّي وَنَصَحْتُ لَكُمْ ۖ فَكَيْفَ آسَىٰ عَلَىٰ قَوْمٍ
كَافِرِينَ ﴿٩٣﴾

94. Na hatukumleta Nabii yoyote katika mji wowote (akakadhibishwa) ila huwatesa wakazi wake kwa taabu na mashaka ili wapate kunyenyekea. (Lakini hawanyenyekei).

وَمَا أَرْسَلْنَا فِي قَرْيَةٍ مِنْ نَبِيٍّ إِلَّا أَخَذْنَا
أَهْلَهَا بِالْبَأْسَاءِ وَالضَّرَّاءِ لَعَلَّهُمْ يَضَّرَّعُونَ ﴿٩٤﴾

95. Kisha hubadilisha "sisi" mahala pa ubaya kwa wema, (Tukawaendoshea balaa zile japo hawajaamini) hata wakazidi (kuneemeka na kuwa wengi) na wakasema: "(Hata zamani ni vivi hivi):–taabu na raha ziliwafikia baba zetu. (Haya si kwa ajili ya kukadhibisha)." Basi Tukawaangamiza kwa ghafla, hali ya kuwa hawajatambua.

ثُمَّ بَدَّلْنَا مَكَانَ السَّيِّئَةِ الْحَسَنَةَ حَتَّىٰ عَفَوْا وَقَالُوا
قَدْ مَسَّ آبَاءَنَا الضَّرَّاءُ وَالسَّرَّاءُ فَأَخَذْنَاهُمْ
بَغْتَةً وَهُمْ لَا يَشْعُرُونَ ﴿٩٥﴾

---

Basi maonyo makubwa baada ya ukafiri wao yalikuwa juu ya wiziwizi wao katika biashara hizo walizokuwa wakizifanya.

Mtume wao huyo—Nabii Shuebu—alikuwa wa kabila moja na wao na akitokana na matajiri na wazalendo wa hapo.

88. Kinaendelea kisa cha Nabii Shuebu na kaumu zake.

94-95. Kuonyesha kutesa kwake Mwenyezi Mungu; kuwa hatesi kwa papara. Huwapa muda hao wabaya wa

96. Na lau kama watu wa miji wangaliamini na kuogopa, kwa yakini tungaliwafungulia baraka za mbingu na ardhi. Lakini walikadhibisha; tukawapatiliza kwa sababu ya yale waliyokuwa wakiyachuma.

97. Je, watu wa miji (hii walio wabaya) wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafikia usiku, hali wamelala?

98. Au watu wa miji (hiyo) wameaminisha ya kuwa adhabu yetu haitawafikia mchana, hali wanacheza?

99. Je, wameaminisha kuadhibiwa na Mwenyezi Mungu? Hawaaminishi adhabu ya Mwenyezi Mungu ila watu ambao (watakuwa) wenye khasara.

100. Je, hawajui hawa waliorithi ardhi baada ya wale wakazi wake (wa zamani walioangamizwa) kwamba tukitaka tutawatia misibani kwa dhambi zao na tutapiga muhuri juu ya nyoyo zao; na kwa hivyo hawatasikia?

101. Hiyo ni miji (mikubwa mikubwa) tunakusimulia baadhi ya habari zake. Na bila shaka Mitume wao waliwafikia kwa hoja zilizo waziwazi. Lakini hawakuwa wenye kuamini waliyoyakadhibisha zamani. Namna hivi Mwenyezi Mungu anazipiga muhuri nyoyo za makafiri.

102. Na kwa wengi wao hatukuona (kutekeleza) ahadi yo yote; bali kwa hakika wengi wao tuliwakuta maasi tu.

103. Kisha baada ya (Mitume hao) tukampeleka Musa na hoja zetu kwa Firauni na watu wake. Lakini walizikataa. Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa waharibifu.

104. Na alisema Musa: "Ewe Firauni! Mimi ni Mtume nitokaye kwa Mola wa walimwengu."

105. "Yanipasa nisiseme juu ya Mwenyezi Mungu (lo lote) ila haki (tu). Kwa yakini nimekufikieni kwa dalili waziwazi zitokazo kwa Mola wenu. Basi wapeleke wana wa Israili pamoja nami (nchi waitakayo, usiwazuilie hapa Misri ukawa unawadhili).

وَلَوْ أَنَّ أَهْلَ الْقُرَىٰ آمَنُوا وَاتَّقَوْا لَفَتَحْنَا
عَلَيْهِم بَرَكَاتٍ مِّنَ السَّمَاءِ وَالْأَرْضِ وَلَٰكِن كَذَّبُوا
فَأَخَذْنَاهُم بِمَا كَانُوا يَكْسِبُونَ ﴿٩٦﴾
أَفَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن يَأْتِيَهُم بَأْسُنَا بَيَاتًا وَهُمْ
نَائِمُونَ ﴿٩٧﴾
أَوَأَمِنَ أَهْلُ الْقُرَىٰ أَن يَأْتِيَهُم بَأْسُنَا ضُحًى وَهُمْ
يَلْعَبُونَ ﴿٩٨﴾
أَفَأَمِنُوا مَكْرَ اللَّهِ ۚ فَلَا يَأْمَنُ مَكْرَ اللَّهِ إِلَّا الْقَوْمُ
الْخَاسِرُونَ ﴿٩٩﴾ ع
أَوَلَمْ يَهْدِ لِلَّذِينَ يَرِثُونَ الْأَرْضَ مِن بَعْدِ
أَهْلِهَا أَن لَّوْ نَشَاءُ أَصَبْنَاهُم بِذُنُوبِهِمْ ۚ وَنَطْبَعُ
عَلَىٰ قُلُوبِهِمْ فَهُمْ لَا يَسْمَعُونَ ﴿١٠٠﴾
تِلْكَ الْقُرَىٰ نَقُصُّ عَلَيْكَ مِنْ أَنبَائِهَا ۚ
وَلَقَدْ جَاءَتْهُمْ رُسُلُهُم بِالْبَيِّنَاتِ فَمَا كَانُوا
لِيُؤْمِنُوا بِمَا كَذَّبُوا مِن قَبْلُ ۚ كَذَٰلِكَ يَطْبَعُ اللَّهُ عَلَىٰ
قُلُوبِ الْكَافِرِينَ ﴿١٠١﴾
وَمَا وَجَدْنَا لِأَكْثَرِهِم مِّنْ عَهْدٍ ۖ وَإِن وَجَدْنَا
أَكْثَرَهُمْ لَفَاسِقِينَ ﴿١٠٢﴾
ثُمَّ بَعَثْنَا مِن بَعْدِهِم مُّوسَىٰ بِآيَاتِنَا إِلَىٰ فِرْعَوْنَ وَمَلَئِهِ
فَظَلَمُوا بِهَا ۖ فَانظُرْ كَيْفَ كَانَ عَاقِبَةُ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٠٣﴾
وَقَالَ مُوسَىٰ يَا فِرْعَوْنُ إِنِّي رَسُولٌ مِّن رَّبِّ الْعَالَمِينَ ﴿١٠٤﴾
حَقِيقٌ عَلَىٰ أَن لَّا أَقُولَ عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ ۚ
قَدْ جِئْتُكُم بِبَيِّنَةٍ مِّن رَّبِّكُمْ فَأَرْسِلْ مَعِيَ
بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٠٥﴾

kuweza kurejea kwake.

96. Kuonyesha ambayo wangeyapata lau wangekwenda mwendo mzuri.

97-99. Kuonyesha mateso ambayo yanaweza kuwafika.

101. Hawakupinga kwa ujinga, lakini walipinga kwa upinzani tu; utadhani nyoyo zao zimepigwa muhuri, haziingii kheri.

103-171. Habari za Nabii Musa na kaumu zake.

106. (Firauni) akasema: "Kama umekuja na hoja, basi ilete ukiwa ni miongoni mwa wasemao kweli."

قَالَ إِن كُنتَ جِئْتَ بِآيَةٍ فَأْتِ بِهَا إِن كُنتَ
مِنَ الصَّادِقِينَ ﴿١٠٦﴾

107. (Hapo Nabii Musa) akaitupa fimbo yake (chini). Na mara ikawa nyoka dhahiri.

فَأَلْقَىٰ عَصَاهُ فَإِذَا هِيَ ثُعْبَانٌ مُّبِينٌ ﴿١٠٧﴾

108. Na akatoa mkono wake. Mara ukawa mweupe kwa watazamao.

وَنَزَعَ يَدَهُ فَإِذَا هِيَ بَيْضَاءُ لِلنَّاظِرِينَ ﴿١٠٨﴾

109. Wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni (pamoja na yeye Firauni): "Hakika huyu ni mchawi ajuaye (uchawi vyema)

قَالَ الْمَلَأُ مِن قَوْمِ فِرْعَوْنَ إِنَّ هَٰذَا
لَسَاحِرٌ عَلِيمٌ ﴿١٠٩﴾

110. Anataka kukutoweni katika ardhi yenu. Basi mnatoa shauri gani?"

يُرِيدُ أَن يُخْرِجَكُم مِّنْ أَرْضِكُمْ ۖ فَمَاذَا تَأْمُرُونَ ﴿١١٠﴾

111. Wakasema: (kumwambia Firauni) "Muwache kidogo yeye na ndugu yake (huyu Haruni anayejipa Utume pamoja naye) usiwaue). Na watume wakusanyao watu mijini (wakukusanyie wachawi wakubwa wakubwa wote),"

قَالُوا أَرْجِهْ وَأَخَاهُ وَأَرْسِلْ فِي الْمَدَائِنِ
حَاشِرِينَ ﴿١١١﴾

112. "Wakuletee kila mchawi ajuaye."

يَأْتُوكَ بِكُلِّ سَاحِرٍ عَلِيمٍ ﴿١١٢﴾

113. Wakaja wachawi kwa Firauni, wakasema: "Tutapata ujira ikiwa tutashinda?"

وَجَاءَ السَّحَرَةُ فِرْعَوْنَ قَالُوا إِنَّ لَنَا لَأَجْرًا
إِن كُنَّا نَحْنُ الْغَالِبِينَ ﴿١١٣﴾

114. Akasema: "Naam, nanyi bila shaka mtakuwa miongoni mwa wanaokaribishwa (kwangu kila wakati)."

قَالَ نَعَمْ وَإِنَّكُمْ لَمِنَ الْمُقَرَّبِينَ ﴿١١٤﴾

115. Wakasema: "Ewe Musa! Je, utatupa wewe (uchawi wako mbele ya watu wauone) au tutakuwa sisi watupao (kwanza)?"

قَالُوا يَا مُوسَىٰ إِمَّا أَن تُلْقِيَ وَإِمَّا أَن نَّكُونَ نَحْنُ
الْمُلْقِينَ ﴿١١٥﴾

116. (Musa) Akasema: "Tupeni." Basi walipotupa waliyazuga macho ya watu na wakawaogopesha, na wakaleta uchawi mkubwa.

قَالَ أَلْقُوا ۖ فَلَمَّا أَلْقَوْا سَحَرُوا أَعْيُنَ النَّاسِ
وَاسْتَرْهَبُوهُمْ وَجَاءُوا بِسِحْرٍ عَظِيمٍ ﴿١١٦﴾

117. Na tukampelekea Wahyi Musa ya kwamba, "Tupa fimbo yako." Mara ikavimeza vyote vile walivyovibuni (wale wachawi).

وَأَوْحَيْنَا إِلَىٰ مُوسَىٰ أَنْ أَلْقِ عَصَاكَ ۖ فَإِذَا هِيَ تَلْقَفُ
مَا يَأْفِكُونَ ﴿١١٧﴾

118. Ukweli ukasimama na yakaharibika waliyokuwa wakiyatenda.

فَوَقَعَ الْحَقُّ وَبَطَلَ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١١٨﴾

---

107. Ilivyokuwa dini yao kukataa miujiza aliyoitaja Mwenyezi Mungu; na hapa katika hii Aya waliyoifanya ya 108 unatajwa muujiza wa kugeuka nyoka fimbo ya Nabii Musa kila akitaka kuonyesha muujiza huo. Na umetajwa muujiza huu katika Qurani nzima. Basi ndiyo wanahangaika hapa, mara wanasema: "Njozi" yaani ndoto. Hatujui akiota nani kuwa hiyo fimbo imegeuka nyoka? Labda Firauni na watu wake walikuwa wakiota tu kuwa hiyo fimbo ya Musa imekuwa nyoka. Mara wanasema: "Kwa kuyafanya macho ya watazamaji waione fimbo katika umbo la nyoka" (yaani lakini haikugeuka khasa kuwa nyoka). Unaona ukafiri wao. Wanakanusha. Wanasema haikuwa fimbo ya Musa ikigeuka nyoka, kisha ikirejea tena kuwa fimbo; na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anamwambia Nabii Musa katika Aya ya 21 ya *Surat Taha: "Sanuiyduhaa Syratahal Uwlaa"* (Sasa hivi tutairudisha hali yake ya kwanza.) ya ufimbo. Na wao wanasema: "Uwongo, haikugeuka katika hali yake ile." Sisi hatujui ukafiri zaidi kuliko wa kumuona Mungu muongo.

Na katika kubabaika kwao wametaja baadhi ya miujiza na karama; na huku wanazita Njozi (ndoto). Wanapapatika kama wafa maji.

119. Kwa hivyo walishindwa hapo, na wakawa wenye kudhalilika.

فَغُلِبُوا هُنَالِكَ وَانْقَلَبُوا صٰغِرِينَ ﴿١١٩﴾

120. Na wachawi wakapinduliwa (wakapinduka) wanasujudu.

وَأُلْقِيَ السَّحَرَةُ سٰجِدِينَ ﴿١٢٠﴾

121. Wakasema: "Tumemuamini Mola wa walimwengu (wote),"

قَالُوا آمَنَّا بِرَبِّ الْعٰلَمِينَ ﴿١٢١﴾

122. "Mola wa Musa na Haruni."

رَبِّ مُوسٰى وَهٰرُونَ ﴿١٢٢﴾

123. Akasema Firauni: "Oh! Mumemuamini kabla sijakuruhusuni? Hii ndiyo hila mliyoifanya mjini (nyinyi na Musa) ili muwatoe humo wenyewe (mkae nyinyi). Lakini mtajua (nini nitakufanyieni)."

قَالَ فِرْعَوْنُ آمَنْتُمْ بِهِ قَبْلَ أَنْ آذَنَ لَكُمْ ۚ إِنَّ هٰذَا لَمَكْرٌ مَكَرْتُمُوهُ فِي الْمَدِينَةِ لِتُخْرِجُوا مِنْهَا أَهْلَهَا ۖ فَسَوْفَ تَعْلَمُونَ ﴿١٢٣﴾

124. "Lazima nitakata mikono yenu na miguu yenu kwa kubadilisha; (mkono wa kulia na mguu wa kushoto utakatwa pamoja; au mkono wa kushoto na mguu wa kulia). Kisha nitakusulubuni nyote (mufe msalabani)."

لَأُقَطِّعَنَّ أَيْدِيَكُمْ وَأَرْجُلَكُمْ مِنْ خِلٰفٍ ثُمَّ لَأُصَلِّبَنَّكُمْ أَجْمَعِينَ ﴿١٢٤﴾

125. Wakasema: "Sisi tutarudi kwa Mola wetu (atatujazi mema)."

قَالُوا إِنَّا إِلٰى رَبِّنَا مُنْقَلِبُونَ ﴿١٢٥﴾

126. "Nawe hukuona baya kwetu sisi lo lote ila kuwa tumeziamini Aya za Mola wetu zilipotufikia. Mola wetu! Tumiminie subira (uvumilivu) na utufishe hali ya kuwa Waislamu."

وَمَا تَنْقِمُ مِنَّا إِلَّا أَنْ آمَنَّا بِآيٰتِ رَبِّنَا لَمَّا جَاءَتْنَا ۚ رَبَّنَا أَفْرِغْ عَلَيْنَا صَبْرًا وَتَوَفَّنَا مُسْلِمِينَ ﴿١٢٦﴾

127. Na wakasema wakuu wa kaumu ya Firauni (kumwambia Firauni): "Je, utamwacha Musa na watu wake walete uharibifu katika nchi na kukuacha wewe na waungu wako (uliosema waabudiwe pamoja na wewe)?" Akasema: "Tutawaua watoto wao wanaume na tutawaacha hai wanawake wao, na bila shaka sisi ni wenye nguvu juu yao."

وَقَالَ الْمَلَأُ مِنْ قَوْمِ فِرْعَوْنَ أَتَذَرُ مُوسٰى وَقَوْمَهُ لِيُفْسِدُوا فِي الْأَرْضِ وَيَذَرَكَ وَآلِهَتَكَ ۚ قَالَ سَنُقَتِّلُ أَبْنَاءَهُمْ وَنَسْتَحْيِي نِسَاءَهُمْ ۚ وَإِنَّا فَوْقَهُمْ قٰهِرُونَ ﴿١٢٧﴾

128. Musa akawaambia kaumu yake: "Ombeni msaada kwa Mwenyezi Mungu na subirini. Ardhi ni ya Mwenyezi Mungu, atamrithisha amtakaye katika waja wake; na mwisho (mwema) ni kwa wamchao."

قَالَ مُوسٰى لِقَوْمِهِ اسْتَعِينُوا بِاللّٰهِ وَاصْبِرُوا ۚ إِنَّ الْأَرْضَ لِلّٰهِ يُورِثُهَا مَنْ يَشَاءُ مِنْ عِبَادِهِ ۖ وَالْعَاقِبَةُ لِلْمُتَّقِينَ ﴿١٢٨﴾

129. Wakasema: "Tumeudhiwa kabla hujatufikia, na (pia sasa) baada ya wewe kutujia." (Musa) akasema: "Asaa Mola wenu atamwangamiza adui yenu na kukufanyeni watawala katika nchi (hizi), na aone jinsi mtakavyofanya."

قَالُوا أُوذِينَا مِنْ قَبْلِ أَنْ تَأْتِيَنَا وَمِنْ بَعْدِ مَا جِئْتَنَا ۚ قَالَ عَسٰى رَبُّكُمْ أَنْ يُهْلِكَ عَدُوَّكُمْ وَيَسْتَخْلِفَكُمْ فِي الْأَرْضِ فَيَنْظُرَ كَيْفَ تَعْمَلُونَ ﴿١٢٩﴾

---

128. Kuonyesha kuwa kusubiri na kutegemea Mwenyezi Mungu na kwenda mwendo mwema ndio sababu ya kutengenekewa duniani na Akhera.

129. Wachawi (Makuhani) wa Firauni walimpa khabari Firauni kuwa atazaliwa kijana mwanamume kwa Mayahudi atakayekuwa sababu ya kuondoka ufalme wao Mafirauni.

130. Na hakika tuliwaadhibu watu wa Firauni kwa miyaka (ya njaa kubwa kabisa) na kwa kupungukiwa na mazao, ili wapate kukumbuka.

131. (Walikuwa hivi): unapowafikia wema husema: "Huu ni kwa ajili yetu." Na ukiwafikia ubaya humnasibishia ukorofi huo Musa na walio pamoja naye. Hakika ukorofi wao (huo unaowafikia) unatoka kwa Mwenyezi Mungu (kwa ajili ya ubaya wao). Lakini wengi katika wao hawajui.

وَلَقَدْ أَخَذْنَا آلَ فِرْعَوْنَ بِالسِّنِينَ وَنَقْصٍ
مِّنَ الثَّمَرَاتِ لَعَلَّهُمْ يَذَّكَّرُونَ ﴿١٣٠﴾
فَإِذَا جَاءَتْهُمُ الْحَسَنَةُ قَالُوا لَنَا هَٰذِهِ ۖ وَإِن
تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَطَّيَّرُوا بِمُوسَىٰ وَمَن مَّعَهُ ۗ
أَلَا إِنَّمَا طَائِرُهُمْ عِندَ اللَّهِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ لَا
يَعْلَمُونَ ﴿١٣١﴾

---

Basi akatoa amri kufatishiwa kila siku nyumba za Mayahudi kutazamwa watoto wanaozaliwa. Akizaliwa mwanamume anachukuliwa papo hapo kwenda kuuawa!

Siku zile zile akazaliwa Nabii Musa. Mama yake asistahimili kungoja kumwona mwanawe anapopotolewa mikononi mwake na maaskari anakwenda kuuawa. Akamtia mwenyewe kisandukuni kwa uzuri, akamtumbukiza mtoni (mikono ya mto wa Nile). Alifanya hivyo ili asukumizike popote atakaposikumizika — Yeye na Bahati yake tena; Kufa au Kupona.

Kwa bahati nzuri alisukumizika mpaka mbele ya Firauni na mkewe walipokuwa wakikoga. Firauni akatoa amri auawe. Mkewe akakataa katakata kumwachia mumewe kumuua. Bali alipitisha deko lake kwa mumewe hata akakubalisha awe mtoto wao wa kulea! Wakamlea kama mtoto wao wa kumzaa; kama tutakavyokuja kuona katika sura za mbele Inshaallah.

Alipokufa Firauni aliyemlea Nabii Musa alitawala Firauni mwengine. Basi alipotawala tu. Firauni huyu—kabla hakutokeza Nabii Musa kwa jina la Utume—aliondosha ile ada ya kuwaua vijana wa Kiyahudi kwani alikwisha kutambua kuwa huyo mtoto wa Kiyahudi anayechelewa kuondosha ufalme wa Kifirauni ni yule aliyelelewa na Firauni aliyekuwa kabla yake, kisha akafanya chungu ya vitendo, na baadaye akakimbia kabla ya huyo Firauni kufa. Akaona lililokuwa likiogopwa kutokea limekwishatokea; hapana faida ya kuwaua waliosalia. Bora awaachie vivyo hivyo wawe watumishi wa kutumika na wawe watu duni wa kutaabika.

Sasa alipotokeza Nabii Musa katika zama zake akafanya haya ya ishara ya kuondosha ufalme wake; basi kwa uchungu wake na ghamidha yake ndiyo akarejeza amri ya kuuawa tena watoto wa Kiyahudi. Hakufanya haya kwa ajili ya kuogopa kutokea Mwangamizaji wao. La. Hakufanya kwa ajili ya haya. Kwani huyu ndiye amekwisha kutokea hivi. Imekuwa sasa anayafanya haya kwa ajili ya kuwaudhi tu hao Mayahudi na kuwazidisha unyonge.

130. Wakati mwengine tamko la *Thamarat* huwa maana yake mtoto. Basi walipatwa na msiba huu pia wa kufiwa na watoto au wa kutozaa kama kawaida yao.

131. Tumeona katika Aya ya 94 ya hii *Suratil Aaraf* kuwa Mwenyezi Mungu huwatia adabu wale wanaowapinga Mitume yake, kisha huwaondoshea; na huwatia tena adabu na huwaondoshea ili watanabahi waone kuwa hayo yanayowafika ni kwa ajili ya ubaya wao wa kumpinga Mtume. Anawafanyia hayo wapate kumuamini wasimpinge.

Basi wale wakubwa wa mji ambao hawapendi mambo yanayoletwa na Mitume huwadaganya watu kwa kuwaambia "Ubaya huu unaotufika ni kwa ajili ya ukorofi wa huyu aliyeleta uzushi huu aliokuja nao na kujipa Utume. Kwanza hatukuona haya kabla hakuja huyu."

Na hawa wakubwa wanajuwa kuwa kwanza hawajaletewa hayo kwa sababu walikuwa hawajaasi bado. Na sasa yanawapata hayo kwa ajili ya maasi yao ya kumpinga huyo Mtume. Lakini wao wanayegeuza chini juu, juu chini, makusudi ili wapate kuzidi kuwatia vitanga vya macho hao wajinga wanaowapoteza maisha; na wenyewe hao wajinga hawatambui masikini, kama alivyosema Mwenyezi Mungu katika mwisho wa Aya hii kuwa: "Lakini wengi katika wao hawajui," wametiwa shemere na hao wakubwa, wanaburutwa tu, na wao wanabururika.

Na maisha wako ulimwenguni watu wa namna mbili hizi. Waongozi wapotofu na wafuasi vipofu. Bwana anasema Hivi; wanajifuatia tu. Au Bwana anafanya Hivi, wanajifuatia tu vile vile.

Makosa makubwa kabisa katika dini kuwa mtu anajifuatia tu wakuu wanavyosema na wanavyofanya pasi na kujua walipoyatoa hayo. Sharti yawe yanatokana na Mwenyezi Mungu na Mtume wake ndiyo yawe ya kufuatwa; siyo yaliyosemwa tu kwa mavurumizo. Hayana ruhusa hayo kufuatwa.

Wala hautakuwa udhuru siku ya Kiyamaa mbele ya Mwenyezi Mungu kusema 'Sikuwa nikijuwa.' Utaambiwa 'Kwa nini usiulize?"

Qurani yote inahimiza mara kwa mara kutaka ujue yakini wewe Mwenyewe, sio kujifuatia tu wanavyojifanyia watu au wanavyojisemea tu; hata wakiwa wakubwa vipi. Mwenyezi Mungu anasema katika Aya ya 36 ya *Sura Bani Israil:* "Wala usifuate (ukipita ukiyasema au ukiyafanya) usio na ilimu (ujuzi) nayo." Na anasema katika Aya

132. Na wakasema (kumwambia Musa): "Ishara yo yote utakayotuletea ili uturoge kwayo (hutafanikiwa, kwani) hatutakuamini."

وَقَالُوا مَهْمَا تَأْتِنَا بِهِ مِنْ آيَةٍ لِتَسْحَرَنَا بِهَا فَمَا
نَحْنُ لَكَ بِمُؤْمِنِينَ ﴿١٣٢﴾

133. Basi tukawapelekea tufani na nzige na vijidudu vinavyobungua na vyura na damu, kuwa ishara zilizopambanuliwa wazi wazi (kuonyesha ukweli wa Nabii Musa); lakini wakatakabari. Na walikuwa watu wabaya (kabisa).

فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمُ الطُّوفَانَ وَالْجَرَادَ وَالْقُمَّلَ
وَالضَّفَادِعَ وَالدَّمَ آيَاتٍ مُفَصَّلَاتٍ
فَاسْتَكْبَرُوا وَكَانُوا قَوْمًا مُجْرِمِينَ ﴿١٣٣﴾

---

ya 43 ya *Suratin Nahl* na Aya ya 7 *Suratil Anbiyaa*: "Basi waulizeni wenye kumbukumbu za vitabu vya Mwenyezi Mungu vya kale ikiwa nyinyi hamjui," msifuate tu!

132. Wanamkatisha tamaa Nabii Musa hata miujiza gani akiwatolea, wao hawatakubali kumfuata na kumkiri kuwa ni Mtume.

133. Yanatajwa baadhi ya masaibu yaliyowapata hao waliompinga Nabii Musa. Na namna yalivyokuwa yakiondoka na kuja.

(a) Kwanza walijiwa na tufani (Kufurika sana ule mto wa Nile mpaka ukavunja).

Mara tu walipoona kishindo hiki walimwendea Nabii Musa kumuomba kwamba akiwaondoshea baa hii watamuamini; kama ilivyotajwa katika Aya ya 134. Nabii Musa akafurahi akaona kuwa labda kweli wataamini. Basi akawaombea. Ikaondoka baa hiyo. Lakini hawakuamini.

Na kwa kufurika kule ule mto yalitapanyika matope mengi ya mbolea mahala pengi pasipopata zamani kufikiwa na mbolea hiyo. Basi kukapandwa hata pasipokuwa pakipandwa. Wakafurahi wale makafiri wakaona hawakudhurika lo lote kwa tufani ile bali wamepata mavuno zaidi. Na wakamsuta Nabii Musa na kumsusuwika.

(b) Basi mara tu mavuno yalipokuwa tayari walishuka nzige wasiopata kuonekana; wanashambulia mavuno makubwa mazuri hayo. Haya mbio makafiri wakamkimbilia Nabii Musaa na vilio vikubwa na unyenyekevu kuwa akiwaondoshea nzige hao basi hapana shaka watasilimu.

Nabii Musa ukalainika moyo wake akawaombea kwa dhati yake. Na pale pale nzige wakaondoka—na hali ya kuwa wamekula kitu chema; lakini walichosaza ni kingi zaidi.

Makafiri walipoona wamesalimikiwa vizuri hivyo walikhalifu waadi wao wakakataa kusilimu.

(c) Mara Mwenyezi Mungu aliwaletea kwa nguvu vile vijidudu vinavyokula mimea na kubungua mazao. Wakaanza kuharibu kweli kweli yale mazao na kwa upesi sana.

Mara wakapiga mbio kwa Nabii Musa na vilio vyao na kutoa ahadi zao wasizozitimiza. Lakini Mitume ni marahimu. Mara hufanya huruma wakasahau yaliyopita nyuma. Basi akawaombea dua kwa dhati yake; na wadudu wakaondoka, kikasalimika kilichosalimika. Nacho si haba; wamebakiwa na cha kufutia machozi.

Basi walikipigia mtindi na walipokivuna wakakataa kusilimu. Basi chakula cha mavuno hayo kiliwatokea Puwani.

(d) Mara siku moja kila tonge wanayoiteka ya chakula chao kilichopikwa kwa mazao yale—kila tonge wakitaka kuitia kinywani inageuka chura. Vyura wanaruka huku na huku! Hicho kifo sasa cha njaa. Kila kinachotaka kutiwa kinywani kinageuka chura. Wakafa waliokufa. Haya mbio hizo kwa Nabii Musa kustajiri na adhabu ya ajabu hii na kutaka waondoshewe; na wao tayari kweli kweli safari hii kuamini.

Nabii Musa akaomba; na adhabu ile ya vyura ikaondoka; na waadi wao wakaurusha. Hawakuamini cho chote. Bali walisema vile vile kama ada yao kuwa huo ni ukorofi wake huyo Musa (kama ilivyobainishwa katika Aya ya 131 ya hii *Suratil Aaraf*). Na husema vile vile kuwa hiyo ndio ada ya ulimwengu—mara mema mara mabaya; na wazee yaliwafika hayo hayo; (kama ilivyobainishwa katika Aya ya 95 ya *Suratil Aaraf*).

(e) Basi baada ya muda tu hivi kila Kinywewa chao wakitaka kukitia kinywani kinageuka damu. Damu, damu nyekundu, mapande kwa mapande. Pasiwe na hila yo yote ya kukifikisha kinywewa kinywani. Hakiwahi kukaa kinywani ila kimekwisha kuwa damu. Basi mambo yametia maji maziwani. Mambo yamepindukia Mipaka.

Hapana pa kukimbilia vile vile ila kwa Nabii Musa. Basi mbio tena hizo moja kwa moja kwa Nabii Musa. Na Nabii Musaa akafanya kazi yake ile ile; na mambo yakatengenea. Na wao wakarejelea yao yale yale waliyoyasema katika Aya ya 132 ya hii *Suratil Aaraf* ya kuwa Hata Viroja gani wakiletewa hawataamini.

Lakini si wote kabisa. Wako wachache sana waliokuwa wakiamini kila Kituko kikija kikaondoka.

134. Na inapowaangukia adhabu husema: "Ewe Musa! Tuombee kwa Mola wako kwa yale aliyokuahidi. Kama ukituondolea adhabu bila shaka tutakuamini na kwa yakini tutawapeleka wana wa Israili pamoja nawe (huko mnakotaka)."

وَلَمَّا وَقَعَ عَلَيْهِمُ الرِّجْزُ قَالُوا يَا مُوسَى ادْعُ لَنَا رَبَّكَ بِمَا عَهِدَ عِنْدَكَ ۚ لَئِنْ كَشَفْتَ عَنَّا الرِّجْزَ لَنُؤْمِنَنَّ لَكَ وَلَنُرْسِلَنَّ مَعَكَ بَنِي إِسْرَائِيلَ ﴿١٣٤﴾

135. Lakini tunapowaondolea adhabu—mpaka muda wao watakaoufikia (wa kutolewa roho au wa kuangamizwa kweli kweli) — mara huvunja ahadi.

فَلَمَّا كَشَفْنَا عَنْهُمُ الرِّجْزَ إِلَىٰ أَجَلٍ هُمْ بَالِغُوهُ إِذَا هُمْ يَنْكُثُونَ ﴿١٣٥﴾

136. Basi tukawalipiza kisasi na tukawazamisha baharini kwa sababu ya kuzikadhibisha Ishara zetu (zote zile) na kwa kutozijali.

فَانْتَقَمْنَا مِنْهُمْ فَأَغْرَقْنَاهُمْ فِي الْيَمِّ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٣٦﴾

137. Na tukawarithisha watu waliokuwa wanaonekana madhaifu (waliokuwa wakionewa; nao ndio hao Bani Israili); (tuliwarithisha miji ya) mashariki ya ardhi na magharibi yake ambayo tuliitia baraka (nyingi miji hiyo). Na likatimia neno jema la Mola wako kwa wana wa Israili; kwa kule kuvumilia kwao. Na tukayaangamiza yale aliyokuwa akiyafanya Firauni na watu wake; na (pia) yale waliyokuwa wakiyajenga.

وَأَوْرَثْنَا الْقَوْمَ الَّذِينَ كَانُوا يُسْتَضْعَفُونَ مَشَارِقَ الْأَرْضِ وَمَغَارِبَهَا الَّتِي بَارَكْنَا فِيهَا ۖ وَتَمَّتْ كَلِمَتُ رَبِّكَ الْحُسْنَىٰ عَلَىٰ بَنِي إِسْرَائِيلَ بِمَا صَبَرُوا ۖ وَدَمَّرْنَا مَا كَانَ يَصْنَعُ فِرْعَوْنُ وَقَوْمُهُ وَمَا كَانُوا يَعْرِشُونَ ﴿١٣٧﴾

138. Na tukawavusha wana wa Israili baharini (wakasalimika na balaa za Firauni) na wakawafikia watu waliokuwa wakiabudu masanamu yao. Wakasema "Ewe Musa! Tufanyie waungu na sisi (yaani masanamu) kama wao walivyo na miungu." (Nabii Musa) Akasema: "Hakika nyinyi ni watu mufanyao ujinga."

وَجَاوَزْنَا بِبَنِي إِسْرَائِيلَ الْبَحْرَ فَأَتَوْا عَلَىٰ قَوْمٍ يَعْكُفُونَ عَلَىٰ أَصْنَامٍ لَهُمْ ۚ قَالُوا يَا مُوسَى اجْعَلْ لَنَا إِلَٰهًا كَمَا لَهُمْ آلِهَةٌ ۚ قَالَ إِنَّكُمْ قَوْمٌ تَجْهَلُونَ ﴿١٣٨﴾

139. "Hawa yataangamia haya waliyo nayo na ni bure waliyokuwa wakiyafanya."

إِنَّ هَٰؤُلَاءِ مُتَبَّرٌ مَا هُمْ فِيهِ وَبَاطِلٌ مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٣٩﴾

140. Akasema: "Je, nikutafutieni mungu badala ya Mwenyezi Mungu, hali yeye amekufadhilisheni juu ya walimwengu wote?"

قَالَ أَغَيْرَ اللَّهِ أَبْغِيكُمْ إِلَٰهًا وَهُوَ فَضَّلَكُمْ عَلَى الْعَالَمِينَ ﴿١٤٠﴾

---

138. Mayahudi kwa kule kukaa miaka mingi Misri walifuata baadhi ya dini ya watu wa Misri. Wakaacha yale ya dini yao ya asili—Waliabudu masanamu yenye Sura za watu na masanamu yenye Sura za ng'ombe na masanamu yenye Sura za jua. Kwani watu wa Misri wa kale waliabudu jua, wakaabudu wafalme wao, wakaabudu ng'ombe na wakaabudu vinginevyo.

Basi Mayahudi baada ya kutoka Misri wakenda Shami waliwaona watu wanaabudu masanamu yao—na wao wamekwishazuiliwa mambo hayo—lakini mshipa wa kuabudu masanamu uliwapiga wakamtaka Nabii Musa awafanyie masanamu ya Sura ya Mungu wawaabudu! Nabii Musa akawalaumu hivyo.

*N.B.*—Na tangu Aya ya 138 Mwenyezi Mungu anawatajia Mayahudi waliokuwa zama za Mtume. Anawatajia ihsani alizowafanyia wazee wao zama za Nabii Musa na kabla yake na baada yake na anawatajia baadhi ya maovu yao waliyoyafanya.

Waongo katika tafsiri ya "*Alyamm*" waliyoitoa katika hii Aya waliyoifanya kuwa ni ya 139. Sijui undani wao nini katika maelezo yao haya ya uwongo. Walisema: "Ingawa neno la *al Bahr* na *al yamm* yanafahamiwa kuwa na maana moja, lakini ni dhahiri ya kuwa Qurani inatumia neno *al yamm* inapoeleza kuzamishwa kwa watu wa Firauni." Waongo. Tamko hii limetumika pia pasina makusudio ya kuzamishwa Firauni au watu wake; kama lilivyotumika katika Aya ya 39 ya *Surat Taha* na katika Aya ya 97 ya hiyo hiyo *Surat Taha* na katika Aya ya 7 ya *Suratul Qasas*. Wanasukuma uwongo tu.

140. Mayahudi zama za Mitume yao—walipokuwa wanakwenda mwendo mzuri Mwenyezi Mungu

141. "Na (kumbukeni) tulipokuokoeni kwa Firauni na watu wake waliokupeni maadhibisho mabaya mabaya. Wakiwaua watoto wenu wanaume na kuwaacha hai wanawake. Na katika hayo ulikuwa mtihani mkubwa uliotoka kwa Mola wenu."

وَإِذْ أَنْجَيْنَاكُمْ مِنْ آلِ فِرْعَوْنَ يَسُومُونَكُمْ
سُوءَ الْعَذَابِ ۚ يُقَتِّلُونَ أَبْنَاءَكُمْ وَيَسْتَحْيُونَ
نِسَاءَكُمْ ۚ وَفِي ذَٰلِكُمْ بَلَاءٌ مِنْ رَبِّكُمْ
عَظِيمٌ ﴿١٤١﴾

142. Na tulimuahidi Musa siku thalathini (afanye ibada moja kwa moja, kisha tumpe Taurati) na tukazitimiza kwa kumi; ikatimia miadi ya Mola wake (ya kwenda kumpa hiyo Taurati) siku arubaini. Na Musa akamwambia ndugu yake, Haruni: "Shika mahali pangu katika (kuwaendesha) watu wangu na utengeneze wala usifuate njia ya waharibifu."

وَوَاعَدْنَا مُوسَىٰ ثَلَاثِينَ لَيْلَةً وَأَتْمَمْنَاهَا بِعَشْرٍ
فَتَمَّ مِيقَاتُ رَبِّهِ أَرْبَعِينَ لَيْلَةً ۚ وَقَالَ مُوسَىٰ
لِأَخِيهِ هَارُونَ اخْلُفْنِي فِي قَوْمِي وَأَصْلِحْ وَلَا
تَتَّبِعْ سَبِيلَ الْمُفْسِدِينَ ﴿١٤٢﴾

143. Na alipofika Musa katika miadi yetu, na Mola wake akazungumza naye, (Musa) alisema: "Mola wangu! Nionyeshe (nafsi yako) ili nikuone." Akasema (Mwenyezi Mungu): "Hutaniona, lakini tazama jabali (lilioko mbele yako). Kama litakaa mahali pake (bila kupasuka na kutawanyika) utaweza kuniona." Basi Mola wake alipojionyesha katika jabali (alipoonyesha baadhi ya ishara zake) alilifanya ni lenye kuvunjikavunjika, na Musa akaanguka hali ya kuzimia. Alipozindukana alisema: "(Naitakidi kuwa) Wewe ndiye Mtukufu, (halimkiniki hilo nililolitaka). Natubu kwako, na mimi ni wa kwanza wa wanaoamini (haya)."

وَلَمَّا جَاءَ مُوسَىٰ لِمِيقَاتِنَا وَكَلَّمَهُ رَبُّهُ قَالَ
رَبِّ أَرِنِي أَنْظُرْ إِلَيْكَ ۚ قَالَ لَنْ تَرَانِي وَلَٰكِنِ
انْظُرْ إِلَى الْجَبَلِ فَإِنِ اسْتَقَرَّ مَكَانَهُ فَسَوْفَ
تَرَانِي ۚ فَلَمَّا تَجَلَّىٰ رَبُّهُ لِلْجَبَلِ جَعَلَهُ دَكًّا وَخَرَّ
مُوسَىٰ صَعِقًا ۚ فَلَمَّا أَفَاقَ قَالَ سُبْحَانَكَ تُبْتُ
إِلَيْكَ وَأَنَا أَوَّلُ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٤٣﴾

144. Akasema (Mwenyezi Mungu): "Ewe Musa! Mimi nimekuchagua juu ya watu wote kwa ujumbe wangu na kwa kusema nawe kwangu. Basi pokeya haya niliyokupa, na uwe miongoni mwa wanaoshukuru."

قَالَ يَا مُوسَىٰ إِنِّي اصْطَفَيْتُكَ عَلَى النَّاسِ
بِرِسَالَاتِي وَبِكَلَامِي فَخُذْ مَا آتَيْتُكَ وَكُنْ
مِنَ الشَّاكِرِينَ ﴿١٤٤﴾

145. Na tukamwandikia katika mbao kila kitu— mauidha (ya kila namna) na maelezo ya kila jambo. "Basi yashike kwa imara na uwaamrishe watu wako wayashike bora haya. Karibuni nitakuonyesheni miji

وَكَتَبْنَا لَهُ فِي الْأَلْوَاحِ مِنْ كُلِّ شَيْءٍ مَوْعِظَةً
وَتَفْصِيلًا لِكُلِّ شَيْءٍ فَخُذْهَا بِقُوَّةٍ وَأْمُرْ

---

aliwafadhilisha kuliko walimwengu wote. Na walipoharibu vibaya vibaya vile walivyoharibu, ikateremka daraja yao kweli kweli mbele ya Mwenyezi Mungu; na vile vile mbele ya viumbe. Hawapendwi na viumbe wo wote. Na hao wanaowadhihirishia mapenzi wakawavutia nafuu, ni siasa tu na kujivutia nafuu wenyewe na kujiondolea madhara wenyewe hao wanaojidai kuwa wanafanya haya kwa ajili ya Mayahudi. Uwongo! Hawafanyi hayo ila kwa maslaha yao wenyewe wenye dola hizo. Na siku watakapoona hapana maslaha juu yao watawatupilia mbali kama anavyotupwa Jongoo na mtiwe [kijiti chake cha kumtupia].

141. Wanaambiwa Mayahudi waliokuwa zama za Mtume. Na muradi ni wazee wao waliokuwa zama hizo. Lakini neema hizo zilizowafika wazee wao ndio kama zimewafika wao kwani kwa kunusurika hao ndio wamepatikana wao.

*N.B.*— Ikisemwa katika Kiarabu *Aali Fulan*, 'Watu wa fulani' tupu pasina kutanguliza kumtaja huyo Fulani basi wakati huo haifai kuwa watu wa fulani bali hufasiriwa hivi: 'Fulani na watu wake,' Kama inavyosemwa katika Kiswahili 'Kina Fulani,' akaingia huyu Fulani mwenyewe na hao wenziwe.

142. Nabii Musa ndiye aliyekuwa mkubwa kwa Utume kuliko Nabii Haruni ingawa Nabii Haruni ni mkubwa kuliko Nabii Musa kwa umri.

قَوْمَكَ يَأْخُذُوا بِأَحْسَنِهَا ۚ سَأُرِيكُمْ دَارَ
الْفَاسِقِينَ ﴿١٤٥﴾

ya wavunjao amri (zetu namna ilivyoharibika na nitakutawalisheni nyinyi)."

سَأَصْرِفُ عَنْ آيَاتِيَ الَّذِينَ يَتَكَبَّرُونَ فِي الْأَرْضِ
بِغَيْرِ الْحَقِّ وَإِن يَرَوْا كُلَّ آيَةٍ لَّا يُؤْمِنُوا بِهَا
وَإِن يَرَوْا سَبِيلَ الرُّشْدِ لَا يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا وَإِن يَرَوْا
سَبِيلَ الْغَيِّ يَتَّخِذُوهُ سَبِيلًا ۚ ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ كَذَّبُوا
بِآيَاتِنَا وَكَانُوا عَنْهَا غَافِلِينَ ﴿١٤٦﴾

146. "Nitawaepusha na (kuzingatia) Aya zangu wale wanaotakabari katika nchi pasipo haki; na ambao kila hoja wanayoiona hawaiamini; na kama wakiiona njia ya uwongofu hawaishiki kuwa ndiyo njia; lakini wakiiona njia ya upotofu (upotevu) wanaishika kuwa ndiyo njia. Hayo ni kwa sababu ya kuzikadhibisha Aya zetu na kuzipuza."

وَالَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَلِقَاءِ الْآخِرَةِ حَبِطَتْ
أَعْمَالُهُمْ ۚ هَلْ يُجْزَوْنَ إِلَّا مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٤٧﴾

147. Na wale waliozikadhibisha Aya zetu na (wakakadhibisha) kukutana na Akhera, amali zao zimeharibika. Kwani watalipwa mengine, ila yale yale waliyokuwa wakiyatenda? (Basi maadamu wanatenda mabaya, watalipwa ubaya wao).

وَاتَّخَذَ قَوْمُ مُوسَىٰ مِن بَعْدِهِ مِنْ حُلِيِّهِمْ عِجْلًا
جَسَدًا لَّهُ خُوَارٌ ۚ أَلَمْ يَرَوْا أَنَّهُ لَا يُكَلِّمُهُمْ وَلَا
يَهْدِيهِمْ سَبِيلًا ۘ اتَّخَذُوهُ وَكَانُوا ظَالِمِينَ ﴿١٤٨﴾

148. Na baada yake (baada ya kuondoka kwake kwenda kupokea Taurati) watu wa Musa walifanya, kwa mapambo yao, ndama—kiwiliwili tu kilichokuwa na sauti (kisichokuwa na roho). (Waliyayusha vyombo vyao vya fedha na dhahabu wakaunda sura ya ndama wamuabudu kwa kuona kuwa Nabii Musa hakuwafanyia sura ya mungu walioitaka). Je, hawakuona ya kwamba yeye (mungu wao huyo ndama) hasemi nao wala hawaongozi njia? (Lakini) walimfanya (tu kuwa mungu) na wakawa wenye kudhulumu (nafsi zao).

وَلَمَّا سُقِطَ فِي أَيْدِيهِمْ وَرَأَوْا أَنَّهُمْ قَدْ ضَلُّوا
قَالُوا لَئِن لَّمْ يَرْحَمْنَا رَبُّنَا وَيَغْفِرْ لَنَا لَنَكُونَنَّ
مِنَ الْخَاسِرِينَ ﴿١٤٩﴾

149. Na walipojuta na wakaona ya kwamba wamekwishapotea, walisema: "Kama hatuturehemu Mola wetu na kutusamehe, bila shaka tutakuwa miongoni mwa walioharibikiwa."

وَلَمَّا رَجَعَ مُوسَىٰ إِلَىٰ قَوْمِهِ غَضْبَانَ أَسِفًا
قَالَ بِئْسَمَا خَلَفْتُمُونِي مِن بَعْدِي ۖ أَعَجِلْتُمْ
أَمْرَ رَبِّكُمْ ۖ وَأَلْقَى الْأَلْوَاحَ وَأَخَذَ بِرَأْسِ أَخِيهِ
يَجُرُّهُ إِلَيْهِ ۚ قَالَ ابْنَ أُمَّ إِنَّ الْقَوْمَ اسْتَضْعَفُونِي

150. Na aliporudi Musa kwa watu wake, hali ya kuwa amekasirika na kuhuzunika (kwa kusikia hayo), alisema: "Unaibu mbaya mumenifanyia nyuma yangu baada ya kuondoka. Je, mumeitangulia amri ya Mola wenu (mkafanya yenu kabla ya kujua atakayokuamrisheni)?" Na akazitupa zile mbao (zilizokuwa zimeandikwa Sharia za dini yake), na akakamata kichwa cha nduguye kukivutia kwake (kama anataka kumpiga kwa ghadhabu iliyomshika), akasema (yule ndugu yake ambaye ni Nabii Haruni):

---

148. Kilichokuwa na Sauti. Yaani walitia vitu ndani ya ndama huyo hata akawa anatoa sauti kama ya ng'ombe au walimweka mweko makhsusi hata ukivuma upepo hivi husikiwa sauti tumboni mwake.

*N.B.*— Wengi sana katika hao kaumu walifanya baya kubwa hili; lakini wengine walidumu na ibada yao ya haki pamoja na Nabii Harun. Na katika hawa wazuri ndiyo Nabii Musa alichagua 70 wende kwenye jabali alilosemezwa Nabii Musa wakawatakie radhi wale wabaya, baada ya kutubu mbele ya Nabii Musa.

150. Katika mwisho wa maelezo ya Aya waliyoifanya kuwa ni ya 151 Makadiyani wamejidai kutaja maana ya tamko la "*Maa*" na kutaka watu warejee Sura 4:70 ili waone ule ukafiri wao wa kumdaia Utume mtu wao ambao huo ni ukafiri, kwani ni kumpinga Mwenyezi Mungu aliyesema katika Qurani· yale yote nzima kuwa Utume walipewa waliokuwa KABLA ya Nabii Muhammad, ukamalizikia kwa Nabii Muhammad. Na tumekwisha kuitaja

وَكَادُوا يَقْتُلُونَنِي ۖ فَلَا تُشْمِتْ بِيَ الْأَعْدَاءَ
وَلَا تَجْعَلْنِي مَعَ الْقَوْمِ الظَّالِمِينَ ﴿١٥٠﴾

"Ewe (ndugu yangu) mwana wa mama yangu! Kwa hakika watu (hawa) wamenidharau (hawakusikiliza maneno yangu); na hata walikaribia kuniua, Basi usiwafurahishe maadui juu yangu, wala usiniweke pamoja na watu (waovu) madhalimu (wa nafsi zao)."

قَالَ رَبِّ اغْفِرْ لِي وَلِأَخِي وَأَدْخِلْنَا فِي رَحْمَتِكَ ۖ
ع وَأَنتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ ﴿١٥١﴾

151. Akasema (Musa): "Mola wangu! Nisamehe mimi na ndugu yangu, na utuingize katika rehema yako, maana wewe ndiye Mwenye kurehemu zaidi kuliko wenye kurehemu (wote)."

إِنَّ الَّذِينَ اتَّخَذُوا الْعِجْلَ سَيَنَالُهُمْ غَضَبٌ مِّن
رَّبِّهِمْ وَذِلَّةٌ فِي الْحَيَاةِ الدُّنْيَا ۚ وَكَذَٰلِكَ نَجْزِي
الْمُفْتَرِينَ ﴿١٥٢﴾

152. Hakika wale waliomfanya ndama (kuwa mungu), zitawafikia ghadabu zinazotoka kwa Mola wao na udhalili (mkubwa) katika maisha yao haya ya dunia; na hivi ndivyo tunavyowalipa wazushi (wa dini).

وَالَّذِينَ عَمِلُوا السَّيِّئَاتِ ثُمَّ تَابُوا مِن بَعْدِهَا وَآمَنُوا
إِنَّ رَبَّكَ مِن بَعْدِهَا لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٥٣﴾

153. Na wale waliofanya mabaya, kisha wakatubu baada yake na kuamini, Mola wako, baada ya haya (mazuri waliyofanya sasa, atawasamehe) kwani yeye ndiye Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَلَمَّا سَكَتَ عَن مُّوسَى الْغَضَبُ أَخَذَ الْأَلْوَاحَ ۖ
وَفِي نُسْخَتِهَا هُدًى وَرَحْمَةٌ لِّلَّذِينَ هُمْ لِرَبِّهِمْ
يَرْهَبُونَ ﴿١٥٤﴾

154. Na zilipotulia ghadhabu za Musa aliziokota zile mbao. Na katika maandiko yake (mbao hizi) ulikuwamo uwongofu na rehema kwa wale wanaomwogopa Mola wao.

وَاخْتَارَ مُوسَىٰ قَوْمَهُ سَبْعِينَ رَجُلًا لِّمِيقَاتِنَا ۖ
فَلَمَّا أَخَذَتْهُمُ الرَّجْفَةُ قَالَ رَبِّ لَوْ شِئْتَ
أَهْلَكْتَهُم مِّن قَبْلُ وَإِيَّايَ ۖ أَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ
السُّفَهَاءُ مِنَّا ۖ إِنْ هِيَ إِلَّا فِتْنَتُكَ تُضِلُّ بِهَا
مَن تَشَاءُ وَتَهْدِي مَن تَشَاءُ ۖ أَنتَ وَلِيُّنَا فَاغْفِرْ
لَنَا وَارْحَمْنَا ۖ وَأَنتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ ﴿١٥٥﴾

155. Na Musa akawachaguwa watu sabiini (waliowazuri) katika kaumu yake kwa miadi yetu (tuliyomwambia awalete hapo jabalini watake radhi kwa makosa yao yaliyofanywa na wale wenziwao wabaya, ya kuabudu ng'ombe). Na ulipowafika mtetemeko mkubwa (wakakaribia kufa) alisema (Nabii Musa): "Mola wangu! Kama ungetaka ungeliwaangamiza wao na mimi zamani (mbele ya wenziwao wote, wapate kuona nafsi zao kuwa wamekufa kwa kudra ya Mwenyezi Mungu si kwa kuwaua mimi). Unatuangamiza kwa sababu ya yale waliyofanya wale wajinga katika sisi? Hayakuwa haya ila ni majaribio yako, kwayo unamwacha akapotea umtakaye. (Nao ni wale waliotajwa katika Aya ya 146) na humuongoa umtakaye. Wewe ndiye Mlinzi wetu. Basi tusamehe na uturehemu. Nawe ndiye bora wa kughufiria."

---

habari hii iangu katika Marejezo ya Aya ya 7 ya *Suratul Faatiha* na ya 4 ya *Suratul Baqarah*. Na tunawaongezea hapa Aya ya 3 ya *Suratush Shuuraa: "Yuuhy Ilayka Wailal Ladhyna Min Qablik"* "Anavyokuletea wahyi (anavyokufunulia) na (anavyowafunulia) wale waliokutangulia." Hakusema: "Na nitawaletea pia Wahyi watakaokuja — au atakayekuja — baada yako." Kwani nini basi Mwenyezi Mungu akaiuficha kutwambia Utume wao?

153. Kuonyesha rehema ya Mwenyezi Mungu juu ya waja wake hata walio waovu.

155. Wengi sana katika hao kaumu walifanya baya kubwa hili; lakini wengine walidumu na ibada yao ya haki pamoja na Nabii Haruni. Na katika hawa wazuri ndiyo Nabii Musa alichagua 70 wende katika jabali

156. "Na utuandikie mema katika dunia hii na katika Akhera. Sisi tunarejea kwako." Akasema (Mwenyezi Mungu): "Adhabu yangu nitamfikishia nimtakaye (katika wabaya hawa na wabaya wengineo, hakuna wa kunizuilia); na rehema yangu inaweza kukienea kila kitu. Lakini nitawaandikia (kweli kweli kabisa) wale wanaojikinga na yale niliyowakataza, na wanaotoa Zaka na wanaoziamini Aya zetu."

وَاكْتُبْ لَنَا فِي هَٰذِهِ الدُّنْيَا حَسَنَةً وَفِي الْآخِرَةِ
إِنَّا هُدْنَا إِلَيْكَ ۚ قَالَ عَذَابِي أُصِيبُ بِهِ
مَنْ أَشَاءُ ۖ وَرَحْمَتِي وَسِعَتْ كُلَّ شَيْءٍ ۚ
فَسَأَكْتُبُهَا لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ وَيُؤْتُونَ الزَّكَاةَ
وَالَّذِينَ هُمْ بِآيَاتِنَا يُؤْمِنُونَ ﴿١٥٦﴾

157. "Ambao wanamfuata Mtume, Nabii aliye Ummy (asiyejua kusoma wala kuandika, na juu ya hivi atafundisha mafundisho hayo ya ajabu ya Uislamu), ambaye wanamuona ameandikwa kwao katika Taurati na Injili ambaye anawaamrisha mema na anawakataza yaliyo mabaya, na kuwahalalishia vizuri na kuwaharimishia vibaya, na kuwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao (yaani Sharia ngumu za zamani na mila za Kikafiri). Basi wale waliomuamini yeye na kumuhishimu na kumsaidia na kuifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye (yaani Qurani) hao ndio wenye kufaulu."

الَّذِينَ يَتَّبِعُونَ الرَّسُولَ النَّبِيَّ الْأُمِّيَّ الَّذِي
يَجِدُونَهُ مَكْتُوبًا عِنْدَهُمْ فِي التَّوْرَاةِ
وَالْإِنْجِيلِ يَأْمُرُهُمْ بِالْمَعْرُوفِ وَيَنْهَاهُمْ
عَنِ الْمُنْكَرِ وَيُحِلُّ لَهُمُ الطَّيِّبَاتِ وَيُحَرِّمُ عَلَيْهِمُ
الْخَبَائِثَ وَيَضَعُ عَنْهُمْ إِصْرَهُمْ وَالْأَغْلَالَ الَّتِي كَانَتْ
عَلَيْهِمْ ۚ فَالَّذِينَ آمَنُوا بِهِ وَعَزَّرُوهُ وَنَصَرُوهُ
وَاتَّبَعُوا النُّورَ الَّذِي أُنْزِلَ مَعَهُ ۙ أُولَٰئِكَ هُمُ
الْمُفْلِحُونَ ﴿١٥٧﴾ ع

158. Sema (Ewe Nabii Muhammad): "Enyi watu! Hakika mimi ni Mtume wa Mwenyezi Mungu kwenu nyinyi nyote; (Mungu) ambaye anao ufalme wa mbingu na ardhi, hapana aabudiwaye (kwa haki) ila yeye; yeye ndiye ahuishaye na ndiye afishaye. Basi Muaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, aliye Nabii Ummy, (asiyejua kusoma na wala kuandika) ambaye humuamini Mwenyezi Mungu na maneno yake. Na mfuateni yeye ili mpate kuongoka."

قُلْ يَا أَيُّهَا النَّاسُ إِنِّي رَسُولُ اللَّهِ إِلَيْكُمْ جَمِيعًا
الَّذِي لَهُ مُلْكُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ ۖ لَا إِلَٰهَ إِلَّا
هُوَ يُحْيِي وَيُمِيتُ ۖ فَآمِنُوا بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ النَّبِيِّ
الْأُمِّيِّ الَّذِي يُؤْمِنُ بِاللَّهِ وَكَلِمَاتِهِ وَاتَّبِعُوهُ
لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ ﴿١٥٨﴾

159. Na katika kaumu ya Musa walikuwako watu wanaoongoza (wenziwao) kwa haki. Na kwa haki hiyo wanafanya insafu.

وَمِنْ قَوْمِ مُوسَىٰ أُمَّةٌ يَهْدُونَ بِالْحَقِّ وَبِهِ
يَعْدِلُونَ ﴿١٥٩﴾

160. Na tuliwagawanya makabila kumi na mbili, mataifa mbali mbali. Na tukamfunulia Musa

وَقَطَّعْنَاهُمُ اثْنَتَيْ عَشْرَةَ أَسْبَاطًا أُمَمًا ۚ وَأَوْحَيْنَا

---

aliosemezewa Nabii Musa wakawatakie radhi wale wabaya, baada ya kutubu mbele ya Nabii Musa.

Watu 70 hawa walipofika huko wakasemezwa na Mwenyezi Mungu walifikwa na mtetemeko wakawa wanachunga husemi matawi ya miti wakati wa dharuba. Nabii Musa akadhani kuwa wanakufa, akashtuka sana akaogopa asije akatuhumiwa na jamaa zao watu 70 hao kuwa yeye kawatafutia sababu ya kufa; hawakufa vivi hivi tu kwa kufikwa na ajali yao.

157. Naye ni Nabii Muhammad (s.a.w.) Tazama wepesi wa dini ya Uislamu. Kufuzu duniani na Akhera. Hapa katika maelezo ya hii Aya waliyoifanya kuwa ya 158 wametia upotofu watakaoutia katika Aya waliyoifanya ni ya 41 ya Sura ya 33 yaani Aya *Wakhaata an Nabiyyina* iliyoko katika *Suratul Ahzab.* Wakajidai kuifasiri hapa — na huko — kwa "Mbora wa Mitume," na hali ya kuwa maana yake "Mwisho wa Mitume." Tutawajibu huko katika Sura hiyo tukijaaliwa.

160. Nabii Musa alipotoka salama Misri na lile jeshi kubwa kabisa la Mayahudi anakuja nao Shamu aliligawa

إِلَىٰ مُوسَىٰٓ إِذِ اسْتَسْقٰىهُ قَوْمُهٗٓ أَنِ اضْرِب بِّعَصَاكَ
الْحَجَرَ ۚ فَانۢبَجَسَتْ مِنْهُ اثْنَتَا عَشْرَةَ عَيْنًا ۚ
قَدْ عَلِمَ كُلُّ أُنَاسٍ مَّشْرَبَهُمْ ۚ وَظَلَّلْنَا عَلَيْهِمُ
الْغَمَامَ وَأَنزَلْنَا عَلَيْهِمُ الْمَنَّ وَالسَّلْوٰى ۚ كُلُوا
مِن طَيِّبٰتِ مَا رَزَقْنٰكُمْ ۚ وَمَا ظَلَمُونَا وَلٰكِن
كَانُوٓا أَنفُسَهُمْ يَظْلِمُونَ ﴿١٦٠﴾

(tukampelekea wahyi) walipomuomba maji watu wake kuwa: "Piga jiwe kwa fimbo yako." Mara zikabubujika humo (jiweni) chemchemu kumi na mbili, na kila watu wakajua mahali pao pa kunywea. Na tukawafunika kwa mawingu (walipokuwa wanakata jangwa wanatoka Misri), na tukawateremshia manna na salwa. (Tukawaambia): "Kuleni vizuri hivi tulivyokupeni." Wala hawakutudhulumu Sisi (walipofanya ushupavu wao), bali wamejidhulumu (wenyewe) nafsi zao.

وَإِذْ قِيلَ لَهُمُ اسْكُنُوا هٰذِهِ الْقَرْيَةَ وَكُلُوا مِنْهَا
حَيْثُ شِئْتُمْ وَقُولُوا حِطَّةٌ وَادْخُلُوا الْبَابَ سُجَّدًا
نَّغْفِرْ لَكُمْ خَطِيٓـٰٔتِكُمْ ۚ سَنَزِيدُ الْمُحْسِنِينَ ﴿١٦١﴾

161. Na (wakumbushe) walipoambiwa: Kaeni katika mji huu (tulikupeni sisi—Bẹitil Muqaddas), na humo kuleni po pote mpendapo na semeni (wakati wa kuingia) "Tufutie dhambi zetu (Ee Mola wetu)," na ingieni katika mlango (wake) kwa unyenyekevu; tutakusameheni makosa yenu (na) tutawazidishia (mema) watendao mema."

فَبَدَّلَ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنْهُمْ قَوْلًا غَيْرَ الَّذِى قِيلَ
لَهُمْ فَأَرْسَلْنَا عَلَيْهِمْ رِجْزًا مِّنَ السَّمَآءِ بِمَا كَانُوا
يَظْلِمُونَ ﴿١٦٢﴾

162. (Lakini) wale waliodhulumu (nafsi zao) miongoni mwao walibadilisha kauli (nyingine) ghairi ya ile waliyoambiwa. Basi tukawapelekea adhabu kutoka mbinguni kwa walivyokuwa wakijidhulumu wenyewe (nafsi zao).

وَسْـَٔلْهُمْ عَنِ الْقَرْيَةِ الَّتِى كَانَتْ حَاضِرَةَ

163. Na waulizeni habari za mji ambao ulikuwa kando ya bahari; (watu wa mji huo) walipokuwa

---

sehemu kumi na mbili; kila sehemu ikawa na wakubwa wake, ili wakubwa hao watazame mambo yao; na wao ndio wamjuvye Nabii Musa mahitajio yao na mengineyo.

Basi waligawiwa kwa kabila zao 12 kwa idadi ya watoto wa Nabii Yaakubu ambaye ndiye akiitwa Israili hata Mayahudi wakaitwa Bani Israili — watoto wa Israili watoto wa Nabii Yaakubu.

Kila wanaotokana na mmoja katika wale watoto 12 wa Nabii Yaakubu wakawa kabila moja.

Mambo mengi ya miujiza miujiza yalitokea katika safari yao hiyo ya kutoka Misri mpaka Shamu.

(a) Moja ni hili la kuwa walikosa maji kabisa; ukakaribia kuteketea uma wote huo. Ulipokuwa tayari kuangamia, Nabii Musa alipewa muujiza wa kulipiga jabali kwa fimbo yake. Alipolipiga tu lilitoa mito 12—huu unakwenda huku, na huo unakwenda kule na ule unaelekea kwengineko na kadhalika. Na kila kabila ikaambiwa itumie mto wake makhsusi—usiwepo ugomvi wala mzozano.

(b) Muujiza mwengine ni kuwa Jua liliwatopea kweli kweli katika kukata majangwa ya Bara Arabu kwenda Shamu. Jua lilikuwa haliwezi kuvumilika tena. Basi hapo Mwenyezi Mungu aliwaletea kiwingu kizuri chepesi cha kuwazuilia na joto la jua, lakini si cha kuwazuilia na mwangaza wake na raha zake na nafuu zake hilo Jua.

(c) Muujiza mwengine ni kuwa Mwenyezi Mungu alikuwa anawateremshia Manna na Salwa. Manna ilikuwa ni kama umande mtamu kabisa unaoganda katika miti kila alfajiri na kunyinyirika kama asali. Na Salwa ni ndege wenye Sura ya ndege Tomboro hawa wanaopatikana makwetu humu. Na kwa kimombasa huitwa Kware. Walikuwa wakiwajia kwa wingi ndege hawa. Basi walikuwa wakiwachinja na kuwala kwa hiyo asali.

Kilikuwa ni chakula kizuri kabisa—ndege wana ladha kweli kweli na asali ina utamu ajabu kabisa.

Lakini kwa ubaya wao walikikataa mwisho wake chakula hiki na wakakichukia, kama ilivyobainishwa katika Aya nyingi. Na moja katika hizo ni Aya ya 61 ya *Suratul Baqarah*. Basi wakaondoshewa chakula kizuri hiki wasikipate tena. Ndiyo maana Mwenyezi Mungu akasema mwisho wa Aya hii kuwa: Kwa walivyokuwa wakijidhulumu wenyewe (nafsi zao).

162. Badala ya kuomba maghufira waanze maisha mazuri kabisa katika hiyo nchi mpya nzuri waliyopewa; badala ya kuomba maghufira walifanya chungu ya madhambi.

163. Mayahudi katika dini yao walikatazwa kufanya kazi yo yote Jumamosi — wawemo ibadani tu. Na Mwenyezi Mungu dasturi yake huwatia mtihanini viumbe vyake aonyeshe waone wenziwao kama watu hao wanatii amri ya Mwenyezi Mungu au hawatii.

wakivunja (Sheria ya) Jumaamosi (ambayo waliambiwa wasifanye kazi katika siku hiyo, wafanye ibada tu. Na kazi yao ilikuwa uvuvi). Samaki wao walipowajia juu juu siku za Jumaamosi zao; na siku isiyokuwa Jumaamosi hawakuwa wakiwajia (hivyo). Basi namna hivyo tuliwatia mtihani kwa sababu ya kuasi kwao.

الْبَحْرِ إِذْ يَعْدُونَ فِي السَّبْتِ إِذْ تَأْتِيهِمْ
حِيتَانُهُمْ يَوْمَ سَبْتِهِمْ شُرَّعًا وَيَوْمَ لَا يَسْبِتُونَ
لَا تَأْتِيهِمْ ۚ كَذَٰلِكَ نَبْلُوهُم بِمَا كَانُوا
يَفْسُقُونَ ﴿١٦٣﴾

164. Na (wakumbushe wakati) baadhi ya watu katika wao waliposema (kuwaonya waliovunja hishima ya Jumaamosi kwa kuvua, na hali yakuwa wamekatazwa; waliposema): "Pana faida gani kuwaonya watu ambao Mwenyezi Mungu atawaua au atawaadhibu kwa adhabu kali (papa hapa)?" Wakasema: "Tupate kuwa na udhuru mbele ya Mola wenu (kuwa tumeonya lakini hatukusikilizwa) na huenda wakaogopa."

وَإِذْ قَالَتْ أُمَّةٌ مِّنْهُمْ لِمَ تَعِظُونَ قَوْمًا ۙ اللَّهُ
مُهْلِكُهُمْ أَوْ مُعَذِّبُهُمْ عَذَابًا شَدِيدًا ۖ
قَالُوا مَعْذِرَةً إِلَىٰ رَبِّكُمْ وَلَعَلَّهُمْ يَتَّقُونَ ﴿١٦٤﴾

165. Basi walipoyapuuza waliyokuwa wakikumbushwa, tuliwaokoa wale waliokuwa wakikataza maovu, na tukawatesa wale waliodhulumu kwa adhabu mbaya kabisa kwa kuasi kwao.

فَلَمَّا نَسُوا مَا ذُكِّرُوا بِهِ أَنجَيْنَا الَّذِينَ يَنْهَوْنَ
عَنِ السُّوءِ وَأَخَذْنَا الَّذِينَ ظَلَمُوا بِعَذَابٍ
بَئِيسٍ بِمَا كَانُوا يَفْسُقُونَ ﴿١٦٥﴾

166. Na walipotakabari wasiache waliyokatazwa, tuliwaambia: "Kuweni manyani madhalilifu."

فَلَمَّا عَتَوْا عَن مَّا نُهُوا عَنْهُ قُلْنَا لَهُمْ كُونُوا
قِرَدَةً خَاسِئِينَ ﴿١٦٦﴾

167. Na (wakumbushe) alipotangaza Mola wako (ya kwamba) atawaletea (Mayahudi) mpaka siku ya Kiama watu ambao watawaadhibu kwa adhabu mbaya. Hakika Mola wako ni Mwepesi wa kuadhibu. Na bila shaka yeye ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu (wakati watu wanaporejea kwake).

وَإِذْ تَأَذَّنَ رَبُّكَ لَيَبْعَثَنَّ عَلَيْهِمْ إِلَىٰ يَوْمِ
الْقِيَامَةِ مَن يَسُومُهُمْ سُوءَ الْعَذَابِ ۗ إِنَّ رَبَّكَ
لَسَرِيعُ الْعِقَابِ ۖ وَإِنَّهُ لَغَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿١٦٧﴾

---

Basi ulikuwako mji mmoja wa Kiyahudi ambao kazi yake kubwa ni Uvuvi. Basi Mwenyezi Mungu aliwaletea mtihani huu. Ikawa ile siku ya Jumaamosi—siku ya kutofanya kazi ndiyo siku ambayo samaki wakifika katika bahari hiyo chekwa wanachezacheza kama mkurumo wa uronda na vidagaa. Kila Jumaamosi ilikuwa hivi. Na siku isiyokuwa ya Jumaamosi hawakuwa wakija hivi.

Mwisho wake wengine hawakuweza kustahamili, waliingia kuvua. Wenziwao walishituka kuwaona wanafanya vile. Basi wengine wakawaendea kuwanasihi na kuwakataza kukhalifu amri ya Mwenyezi Mungu vile dhahir shahir. Na wengine walikasirika tu lakini wasiwaambie lo lote wale wabaya ila wakiwaambia wale watu wema wanaojitaabisha kuwasemeza wale wabaya, wakiwaambia kama ilivyo katika Aya ya 164 ya hii *Suratil Aaraf:* — "Kwa nini mnawaonya . . ."

Basi ilipokuja amri ya Mwenyezi Mungu ya kuadhibiwa wale waliovua waliadhibiwa barabara kama ilivyotajwa katika Aya ya 165. Na wale wasiokataza walipata adhabu yao nao. Waliosalimika ni wale waliokataza tu, kama ilivyobainishwa katika Aya hiyo hiyo ya 165.

Basi kuwakabili wabaya na kuwakataza ubaya wao ni lazima; haitoshelezi kuchukiwa tu pasi na kuwaambia. Waislamu lazima waamrishane mema na kukatazana mabaya; sio kila mtu kuwa na lake, halimkhusu la mwenzake. Islamu wote ni kitu kimoja. Umoja, Umoja, Umoja.

166. Wengine wanasema hii ndiyo adhabu kali waliotiwa wavuvi. Nao ni kugeuzwa manyani na yakafa baada ya siku mbili tatu, asisalie hata mmoja. Sio hawa manyani tunaowaona. Hawa walikuwako kabla ya hapo.

167. Walionywa Mayahudi tangu zamani kuwa kila wakifanya maovu yao hayo makubwa wanayoyazusha kila mara, basi Mwenyezi Mungu atawasalitishia watu wenye nguvu wawatie adabu barabara.

168. Na tuliwafarikisha (Mayahudi) katika ulimwengu makundi mbali mbali; (lakini) wako katika wao watu walio wema, na wengine katika wao (ambao ndio wengi kabisa) ni kinyume cha hao. Tukawafanyia mitihani mingi kwa mema na mabaya ili wapate kurejea. (Lakini wapi! Hawakutengenea).

169. Basi wakawaandamia nyuma yao (yaani baada ya wale Mayahudi wazuri, Mitume na wengineo, kikaja) kizazi kibaya walioirithi Kitabu (cha Mwenyezi Mungu pasipo kukifuata wala kuzingatia yale ambayo yaliwafika wabaya wao). Wanachukua vilivyokatazwa vya hapa ulimwenguni, na huku wanasema: "Tutasamehewa." Na kama vyengine vya namna hii vikiwafikia pia wanavichukua. Je, hawakufanyiwa ahadi katika Kitabu ya kwamba hawatasema kumnasibishia Mwenyezi Mungu ila ya haki tu? (Na juu ya hivi wanasema uwongo huo kuwa Mungu atawasamehe juu ya ubaya wao huo). Nao wamekwishasoma yaliyomo humo (vitabuni). Na nyumba ya Akhera itawakalia vizuri wale wanaoogopa (wakajiepusha na makatazo ya Mwenyezi Mungu). Je, Hamfahamu?

وَقَطَّعْنٰهُمْ فِي الْأَرْضِ أُمَمًا ۚ مِنْهُمُ الصّٰلِحُوْنَ وَ
مِنْهُمْ دُوْنَ ذٰلِكَ ۖ وَبَلَوْنٰهُمْ بِالْحَسَنٰتِ وَالسَّيِّاٰتِ
لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿١٦٨﴾

فَخَلَفَ مِنْۢ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ وَّرِثُوا الْكِتٰبَ
يَأْخُذُوْنَ عَرَضَ هٰذَا الْأَدْنٰى وَ يَقُوْلُوْنَ
سَيُغْفَرُ لَنَا ۚ وَإِنْ يَّأْتِهِمْ عَرَضٌ مِّثْلُهٗ
يَأْخُذُوْهُ ۚ أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِّيْثَاقُ الْكِتٰبِ
أَنْ لَّا يَقُوْلُوْا عَلَى اللّٰهِ إِلَّا الْحَقَّ وَدَرَسُوْا مَا فِيْهِ
وَالدَّارُ الْاٰخِرَةُ خَيْرٌ لِّلَّذِيْنَ يَتَّقُوْنَ ۚ أَفَلَا
تَعْقِلُوْنَ ﴿١٦٩﴾

---

Basi dola zote zilizokuwa karibu nao ziliwatia adabu tangu hizo zama za zama na mpaka hivi karibuni na mpaka Kiama; ila watengenee. Wakitiwa adabu kali kabisa. Dola za kizamani kabisa huko za Iraqi ziliwatia adabu, dola ya Misri ya Mafirauni iliwatia adabu, dola ya Kifursi ya zama hizo iliwatia adabu, dola ya Magirigi na ya Warumi ziliwatia adabu; dola za Bara Arabu ziliwatia adabu, dola za Ulaya ziliwatia adabu sana khasa dola ya Spain na Rusi. Na hivi juzi tuliona namna dola ya Kijarumani ilivyowafanya. Na hivi wamekwishakuwa tayari kupata adabu nyingine. Lakini uma kirongwe huo, hawendi ila kwa kutiwa adabu.

168. Mayahudi baada ya kuwa uma mmoja wenye nguvu kubwa na ufalme mashuhuri kama huo wa Nabii Daudi na Nabii Sulemani usiopata kuonekana. Basi baada ya ufalme huo walitawanyika ulimwengu, mzima—wadhalilifu—hawana cha kuwakusanya pamoja, la nchi wala ufalme wala dini wala lo lote lile moja wapo la kuwakusanya.

Ikawa kuna Mayahudi Waarabu, Mayahudi Machina, Mayahudi Wazungu, Mayahudi . . .

Ati sasa wanataka wawapatie nchi watu ambao wamekwishaandikiwa kuwa hawatakuwa na nchi. Mbio za Mwana wa Darini tu hizo tunazoziona. Hautapita muda mrefu ila wataporomoka chini: Inshaallah; wawe kama walivyokuwa—hawana Kwao.

169. Sifa hii ya Mayahudi wabaya ya kufanya uovu bila ya kujali kwa kutaraji kusamehewa juu ya ubaya wao huo; sifa hiyo imerithiwa na baadhi ya Waislamu sasa. Kuna chungu ya Waislamu—na wengineo katika wao ni wajuzi wa dini—wanaodhulumu huku na kufisidi huku, wakiambiwa wanasema 'Mwenyezi Mungu Ghafur.' Uwongo maneno haya; na Mwenyezi Mungu anayakataa hapa kama alivyoyakataa mahala pengi kabisa penginepo kama katika Aya ya 17 na 18 za *Suratin Nisaa*. Na Mtume pia amekanusha habari hii.

Hii ni itikadi mbaya tuliyowafuata Mayahudi. Na kuna mengineyo pia tuliowafuata Mayahudi na Manasara na wenye dini nyinginezo.

Na Mtume aliwambia haya kuwa tutapotea baadhi yetu; tutafuata itikadi na nyendo za watu wenye dini nyengine tuache itikadi za dini yetu na njia yake iliyonyoka. Alisema haya Mtume kwa lafdhi hizi: "Mtafuata nyendo za wale waliokuwa kabla yenu. Mtawafuata shubiri kwa shubiri. Hata lau wangeingia katika shimo la kenge basi na nyinyi mtaingia" Kama mambo haya ya kujitumainisha uwongo, mambo ya Kukumbusha misiba (hauli) na Kuacha yaliyo muhimu wakashughulikia ya upuzi.

Na kila Aya zilizowateremkia makafiri basi na wabaya hawa wanaowafuata zinawachukua. Husemwa hivi ndani ya vitabu. Husemwa: "Kila Aya iliyowateremkia makafiri basi huwakokota na maasi wa Kiislamu." Basi natutahadhari na kutupa mwendo wetu na itikadi zetu za Kiislamu.

وَالَّذِيْنَ يُمَسِّكُوْنَ بِالْكِتٰبِ وَاَقَامُوا الصَّلٰوةَ ؕ
اِنَّا لَا نُضِيْعُ اَجْرَ الْمُصْلِحِيْنَ ﴿١٧٠﴾

170. Na wale wanaokishika Kitabu (cha Mwenyezi Mungu kweli kweli) na wakasimamisha Sala, (tutawalipa mema). Hakika sisi hatupotezi malipo ya wafanyao mema.

وَاِذْ نَتَقْنَا الْجَبَلَ فَوْقَهُمْ كَاَنَّهٗ ظُلَّةٌ وَّظَنُّوْٓا
اَنَّهٗ وَاقِعٌۢ بِهِمْ ۚ خُذُوْا مَآ اٰتَيْنٰكُمْ بِقُوَّةٍ
وَّاذْكُرُوْا مَا فِيْهِ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُوْنَ ﴿١٧١﴾

171. Na (wakumbushe), tulipoung'oa mlima (tukaunin'giniza) juu yao kama kwamba ni kiwingu (kilichowafunika), na wakadhani ya kwamba utawaangukia. (Tukawaambia): "Shikeni kwa nguvu (hayo) tuliyokupeni na yakumbukeni yaliyomo ili mpate kuogopa."

وَاِذْ اَخَذَ رَبُّكَ مِنْۢ بَنِيْٓ اٰدَمَ مِنْ ظُهُوْرِهِمْ
ذُرِّيَّتَهُمْ وَاَشْهَدَهُمْ عَلٰٓى اَنْفُسِهِمْ ۚ اَلَسْتُ
بِرَبِّكُمْ ؕ قَالُوْا بَلٰى ۛۚ شَهِدْنَا ۛۚ اَنْ تَقُوْلُوْا يَوْمَ
الْقِيٰمَةِ اِنَّا كُنَّا عَنْ هٰذَا غٰفِلِيْنَ ﴿١٧٢﴾

172. Na (kumbuka) Mola wako alipowaleta katika wanaadamu kutoka migongoni mwao kizazi chao, na akawashuhudisha juu ya nafsi zao (akwaambia): "Je, Mimi siye Mola wenu?" Wakasema: "Ndiye; tunashuhudia (kuwa wewe ndiye Mola wetu)." (Akawaambia Mwenyezi Mungu): "Msije mkasema siku ya Kiyama kuwa sisi tulikuwa tumeghafilika na hayo (hatuyajui)"

اَوْ تَقُوْلُوْٓا اِنَّمَآ اَشْرَكَ اٰبَآؤُنَا مِنْ قَبْلُ وَكُنَّا
ذُرِّيَّةً مِّنْۢ بَعْدِهِمْ ۚ اَفَتُهْلِكُنَا بِمَا فَعَلَ
الْمُبْطِلُوْنَ ﴿١٧٣﴾

173. "Au mkasema, Baba zetu ndio walioshirikisha zamani, nasi tulikuwa kizazi nyuma yao, basi utatuangamiza kwa sababu ya yale waliyoyafanya waovu?" (Hamuwezi kusema haya kwani nyote tumekufahamisheni, nyinyi na wao).

وَكَذٰلِكَ نُفَصِّلُ الْاٰيٰتِ وَلَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ﴿١٧٤﴾

174. Na namna hivi tunazipambanua Aya (zetu) kwa kutaraji kuwa watarejea.

وَاتْلُ عَلَيْهِمْ نَبَاَ الَّذِيْٓ اٰتَيْنٰهُ اٰيٰتِنَا
فَانْسَلَخَ مِنْهَا فَاَتْبَعَهُ الشَّيْطٰنُ فَكَانَ
مِنَ الْغٰوِيْنَ ﴿١٧٥﴾

175. Na wasomee habari za wale tuliowapa Aya zetu (kuzijua), kisha wakajivua nazo (wasizifuate). Na shetani akawaandama, wakawa miongoni mwa waliopotea. (Wasomee habari za wabaya pia wazijue wajiepushe nazo).

وَلَوْ شِئْنَا لَرَفَعْنٰهُ بِهَا وَلٰكِنَّهٗٓ اَخْلَدَ اِلَى
الْاَرْضِ وَاتَّبَعَ هَوٰىهُ ۚ فَمَثَلُهٗ كَمَثَلِ الْكَلْبِ ۚ
اِنْ تَحْمِلْ عَلَيْهِ يَلْهَثْ اَوْ تَتْرُكْهُ يَلْهَثْ ؕ
ذٰلِكَ مَثَلُ الْقَوْمِ الَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا ۚ
فَاقْصُصِ الْقَصَصَ لَعَلَّهُمْ يَتَفَكَّرُوْنَ ﴿١٧٦﴾

176. Na kama tungelitaka tungeliwanyanyua kwazo, lakini wao waligandamana na ardhi (kutaka ukubwa wa Kidunia wakayatupa ya Akhera) na wakayafuata matamanio yao. Basi hali yao ni kama hali ya mbwa; ukimpigia kelele (hukimbia na huku) anahema, na ukimwacha pia huhema. Hiyo ndiyo hali ya watu waliozikadhibisha Aya zetu. Basi simulia hadithi, huenda wakatafakari.

---

171. Mayahudi walipopewa Kitabu cha Taurati waliziona hukumu zake kuwa ni ngumu wakakataa kuzifuata. Nabii Musa aliwashikilia kweli kweli; wasikubali.

Basi Mwenyezi Mungu aliung'oa mlima mmoja mkubwa kabisa akauning'niza juu ya mji ule, wakaambiwa Nawakiri au utawaangukia sasa hivi uwasagesage. Hapo walipoona Kweli Imedhihiri, Uwongo Umejitenga, ndipo walipokubali.

172. Muradi wa Aya hii ni kuwa Mwenyezi Mungu amemtia kila Binaadamu ujuzi wa kujitambua kuwa yeye ameumbwa, na yuko aliyemuumba, na huyo ndiye Mwenyezi Mungu. Basi hana hoja ya kusema kuwa alipotezwa na wazee wake wala nani. Si hoja hiyo kwani kila mmoja amepewa akili na utambuzi. Kwa nini anajifuatia tu.

176. Wanavyuoni wanaojua wakatupa mwendo wao wa dini wakawa chini ya wenye satuwa hapa duniani, wanawaramba na kuwanyenyekea—wakayaacha ya dini kwa ajili ya dunia—ni kama mbwa kweli, udhalilifu

177. Uovu ulioje wa mfano wa wanaozikadhibisha Aya zetu na wakajidhulumu nafsi zao (wenyewe)! (Wanapigiwa mfano na mbwa!)

سَاءَ مَثَلًا الْقَوْمُ الَّذِينَ كَذَّبُوا بِآيَاتِنَا وَ
أَنفُسَهُمْ كَانُوا يَظْلِمُونَ ﴿١٧٧﴾

178. Atakaowaongoza Mwenyezi Mungu ndio watakaoongoka; na atakaowaachia kupotea (kwa kuwa hawafuati anavyowaambia Mwenyezi Mungu, hao) ndio watakaopata khasara.

مَن يَهْدِ اللَّهُ فَهُوَ الْمُهْتَدِي ۖ وَمَن يُضْلِلْ
فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْخَاسِرُونَ ﴿١٧٨﴾

179. Na bila shaka tumewaumbia moto wa Jahannamu wengi katika majini na wanadamu (kwa sababu hii): Nyoyo wanazo, lakini hawafahamu kwazo (Hawataki kufahamu kwazo), na macho wanayo, lakini hawaoni kwayo, na masikio wanayo, lakini hawasikii kwayo. Hao ni kama wanyama; bali wao ni wapotofu (wapotevu) zaidi. Hao ndio walioghafilika.

وَلَقَدْ ذَرَأْنَا لِجَهَنَّمَ كَثِيرًا مِّنَ الْجِنِّ
وَالْإِنسِ ۖ لَهُمْ قُلُوبٌ لَّا يَفْقَهُونَ بِهَا ز
وَلَهُمْ أَعْيُنٌ لَّا يُبْصِرُونَ بِهَا ز وَلَهُمْ آذَانٌ
لَّا يَسْمَعُونَ بِهَا ۚ أُولَٰئِكَ كَالْأَنْعَامِ بَلْ هُمْ أَضَلُّ ۚ
أُولَٰئِكَ هُمُ الْغَافِلُونَ ﴿١٧٩﴾

180. Na Mwenyezi Mungu ana majina mazuri mazuri; muombeni kwayo. Na waacheni wale wanaoharibu utakatifu wa majina yake. Karibuni hivi watalipwa yale waliyokuwa wakiyatenda.

وَلِلَّهِ الْأَسْمَاءُ الْحُسْنَىٰ فَادْعُوهُ بِهَا ۖ وَذَرُوا
الَّذِينَ يُلْحِدُونَ فِي أَسْمَائِهِ ۚ سَيُجْزَوْنَ
مَا كَانُوا يَعْمَلُونَ ﴿١٨٠﴾

---

umewaandama, wanapita wakifuata na huku wanahema.

178. Tumeisema kwa urefu katika Aya 152 ya *Suratul An-am* (Juzuu ya Saba).

179. Hapa wanatajwa watu wa Motoni. Na sababu ya kutiwa kwao Motoni ni hiyo iliyotajwa; siyo wameonewa na Mwenyezi Mungu. Sababu yake ni hiyo; kuwa wamepewa ala (vitu) za kutambua haki—waifuate—na kuitambua batili, waiepuke. Nao hawataki. Basi hii ndiyo sababu ya kutiwa Motoni. Mwenyezi Mungu hawaonei viumbe vyake. Anawapitishia uadilifu wote.

180. Naam Mwenyezi Mungu ana majina yake (Sifa zake) nzuri kabisa kama:—

Aliyejaa Rehema: *Arrahman;* anayewamiminia hiyo Rehema viumbe vyake: *Arrahym,* Hizi ni baadhi ya tafsiri za: *Arrahman Arrahym;* Anayewastahmilia viumbe vyake; hawatesi upesi: *Al Halym;* Mwenye kuwasamehe: *Al Ghafur;* Mwenye kuwapenda: *Al Wadud;* Mwenye kuwapa salama: *Assalam;* Mwenye kuwahifadhi: *Al Muhayamin;* Mwenye kuwaruzuku: *Ar Razzaq.*

Na yako kama haya na mengineyo, mengi sana. Na yaliyo mashuhuri zaidi ni 99.

Basi Mwenyezi Mungu anapenda unapomuomba uwe katika dua yako unayataja majina hayo kwa Mnasaba wa ile haja uiombayo. Ukiwa unamuomba msamaha tumia jina la: *Al Ghafur;* Ukiwa unamwomba salama tumia jina la *Assalam;* Na kama hivi; kama ilivyo katika ile dua ya *Tayyibal Asmaa;* na dua ya *Bismil Ilahi;* ya Sheikh Yusufun Nabhany au dua *Bika Tahassant* ya Sheikh Muhyiddinil Araby; na kama hizi nyingi kabisa ziko. Lakini watu wanazipuza. Wanaona dua kubwa ni kumuomba Mwenyezi Mungu kwa majina ya *Ahl Badr* na majina ya watu wengine, wakawa wanasema:— 'Tunakuomba kwa jaha ya Bwana Fulani, na jaha ya Bwana Fulani na jaha ya . . .!' Badala ya kusema:— 'Tunakuomba kwa kuwa wewe Ndiye Mwenye rehema juu yetu, Mwenye . . .' kama alivyosema Mwenyewe Mwenyezi Mungu katika Aya hii na katika Aya nyinginezo, kama Aya ya 110 ya *Surati Bani Israil.*

Bali kuna wengine hata hawamwambii Mwenyezi Mungu hivyo: "Tunakuomba kwa Fulani utufanyie . . ." Bali humwomba huyo Fulani moja kwa moja wakasema:— "Ewe Bwana Fulani! Mimi sina mwengine ila wewe! Dhiki imenibana kila upande. Matumainio yangu yako kwako. Simtegemei mwengine ila wewe"! Haifai dua hizi.

Na katika walioharibu utakatifu wa majina ya Mwenyezi Mungu ni hao Maqureshi na Waarabu wenziwao waliokuwa wakiyaabudu masanamu na wakiwaitakidi kuwa ni waungu wanawake, ima wake zake Mwenyezi Mungu au watoto wake. Walilichukua jina la Mwenyezi Mungu la ALLAH, yaani Mwenyezi Mungu, wakampa

181. Na katika wale Tuliowaumba wako watu wanaoongoza (wenziwao) kwa haki na wanafanya uadilifu kwa hiyo haki. (Hawakosekani watu hawa ulimwenguni japo ni wachache).

وَمِمَّنْ خَلَقْنَآ أُمَّةٌ يَّهْدُوْنَ بِالْحَقِّ وَبِهٖ
يَعْدِلُوْنَ ﴿١٨١﴾

182. Na wale waliokadhibisha Aya zetu, tutawavuta kidogo kidogo (waingie mikononi mwetu—adhabuni) kwa namna ambayo wenyewe hawajui (kuwa ndio kutiwa mkononi huko).

وَالَّذِيْنَ كَذَّبُوْا بِاٰيٰتِنَا سَنَسْتَدْرِجُهُمْ
مِّنْ حَيْثُ لَا يَعْلَمُوْنَ ﴿١٨٢﴾

183. Nami nitawapa muda (hao wabaya, sitawalipa upesi upesi). Hakika nguvu zangu ni madhubuti (barabara).

وَاُمْلِيْ لَهُمْ ۚ اِنَّ كَيْدِيْ مَتِيْنٌ ﴿١٨٣﴾

184. Je, hawafikiri (wakaona kuwa) mtu wao huyo (yaani Nabii Muhammad) hana wazimu? Hakuwa yeye ila ni muonyaji aliye dhahiri.

اَوَلَمْ يَتَفَكَّرُوْا ۗ مَا بِصَاحِبِهِمْ مِّنْ جِنَّةٍ ۗ اِنْ
هُوَ اِلَّا نَذِيْرٌ مُّبِيْنٌ ﴿١٨٤﴾

185. Je, hawatazami ufalme wa mbingu na ardhi na vitu alivyoviumba Mwenyezi Mungu? Na (hawatazami wakarejea kwa Mungu kwa kuona) kuwa pengine ajali yao iko karibu. Basi baada ya maneno haya hadithi gani nyingine watakayoiamini?

اَوَلَمْ يَنْظُرُوْا فِيْ مَلَكُوْتِ السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ وَمَا
خَلَقَ اللّٰهُ مِنْ شَيْءٍ ۙ وَّاَنْ عَسٰٓى اَنْ يَّكُوْنَ
قَدِ اقْتَرَبَ اَجَلُهُمْ ۚ فَبِاَيِّ حَدِيْثٍۢ بَعْدَهٗ يُؤْمِنُوْنَ ﴿١٨٥﴾

186. Ambao Mwenyezi Mungu anawaachia kupotea (kwa kuwa hawataki kusikiliza), basi hawana mwongozi. Na (Mwenyezi Mungu) anawaacha katika upotofu (upotevu) wao wakitangatanga ovyo.

مَنْ يُّضْلِلِ اللّٰهُ فَلَا هَادِيَ لَهٗ ۚ وَيَذَرُهُمْ فِيْ
طُغْيَانِهِمْ يَعْمَهُوْنَ ﴿١٨٦﴾

187. Wanakuuliza juu ya Saa hiyo (yaani Kiama) kutokea kwake kutakuwa lini? Sema: "Ilimu yake (kuja kwake) iko kwa Mola wangu (tu). Hakuna wa kuidhihirisha kwa wakati wake ila Yeye (tu). Ni nzito katika mbingu na ardhi (imefichikana haijulikani kote huko). Haitakufikieni ila kwa ghafla (tu hivi)." Wanakuuliza kama kwamba wewe uliitafuta (ukaijua). Sema: "Ilimu yake iko kwa

يَسْــَٔلُوْنَكَ عَنِ السَّاعَةِ اَيَّانَ مُرْسٰىهَا ۗ قُلْ
اِنَّمَا عِلْمُهَا عِنْدَ رَبِّيْ ۚ لَا يُجَلِّيْهَا لِوَقْتِهَآ اِلَّا هُوَ ؔ
ثَقُلَتْ فِي السَّمٰوٰتِ وَالْاَرْضِ ۗ لَا تَاْتِيْكُمْ اِلَّا بَغْتَةً ۗ
يَسْــَٔلُوْنَكَ كَاَنَّكَ حَفِيٌّ عَنْهَا ۗ قُلْ اِنَّمَا عِلْمُهَا

---

sanamu lao la kike; wakalita *Allaata* yaani mwenyezi mungu mwanamke. Na wakachukua jina la Mwenyezi Mungu la *Al Aziz;* Mwenye enzi yote mkononi mwake; wakalita sanamu lao la kike *Al Uzza.* Na wakachukua jina la Mwenyezi Mungu la *Al Mannaan;* Mwenye neema kubwa kabisa juu ya viumbe vyake; wakalita sanamu lao la kike *Manah.* Tazama Aya ya 35 ya *Saratul Maida.*

184. Waswahili wanasema 'Akutukanaye hakuchagulii' Atakuvurumizia tusi lo lote lile japo halina uelekeo wo wote na wewe; muradi akutie doa tu.

Basi Maqureshi walimsambikizia Mtume chungu ya sifa mbaya mbaya kama kumwambia mchawi, mzushi, mwenye kurogwa, mwendawazimu.

Ndiyo Mwenyezi Mungu anawatahayarisha hapa kwa kuwaambia hawafikiri kwanza la kumsambikizia mtu? Wanamsambikizia hata ambalo hawatasadikiwa wakimsambikizia nalo? Kama hivyo kumwambia Mtume kuwa mwendawazimu. Kila atakayemuona Mtume atajua kuwa maneno hayo ni uwongo kabisa. Kwani hakuwa na maneno ya kiwazimu wala vitendo vya kiwazimu. Basi ndiyo maana vile vile Mwenyezi Mungu akawasimanga katika Aya ya 32 ya *Surat Tur* kwa kusema "Au hizo akili zao kubwa (wanazojisifu kwazo) ndizo zinazowaamrisha kusema maneno haya (yasiyokuwa na akili)?" Basi wanajitoa maanani kwani wataonekana kuwa wendawazimu ni wao.

Mwenyezi Mungu (tu)." Lakini watu wengi hawajui (wanafuata tu wale wapotezi wao, wakubwa wao).

عِندَ اللَّهِ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لَا يَعْلَمُونَ ﴿١٨٧﴾

188. Sema: "Sina mamlaka ya kujipa nafuu wala ya kujiondolea madhara ila apendavyo Mwenyezi Mungu; na lau kama ningalijua ghaibu ningejizidishia mema mengi; wala isingalinigusa dhara; mimi si cho chote ila ni muonyaji na mtoaji wa habari njema kwa watu wanaoamini."

قُل لَّا أَمْلِكُ لِنَفْسِي نَفْعًا وَلَا ضَرًّا إِلَّا
مَا شَاءَ اللَّهُ ۚ وَلَوْ كُنتُ أَعْلَمُ الْغَيْبَ لَاسْتَكْثَرْتُ
مِنَ الْخَيْرِ وَمَا مَسَّنِيَ السُّوءُ ۚ إِنْ أَنَا إِلَّا نَذِيرٌ
وَبَشِيرٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿١٨٨﴾

189. Yeye ndiye aliyekuumbeni katika nafsi moja; na katika (nafsi) hiyo amewaumba wake wao, ili (kila mwanamume) apate utulivu kwake (mkewe) Na anapoingiliana naye hushika mimba (ambayo huwa) nyepesi na kutembea nayo (yule mwanamke bila ya uzito). (Hata) anapokuwa mja mzito (mimba pevu inamtaabisha), wote wawili (mke na mume)

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُم مِّن نَّفْسٍ وَاحِدَةٍ وَجَعَلَ
مِنْهَا زَوْجَهَا لِيَسْكُنَ إِلَيْهَا ۖ فَلَمَّا تَغَشَّاهَا
حَمَلَتْ حَمْلًا خَفِيفًا فَمَرَّتْ بِهِ ۖ فَلَمَّا أَثْقَلَت

---

187. Mwaka khasa wa kufika Kiyama au mwezi wake au wiki yake au siku yake au saa yake, hakuna anayejua ila Mwenyewe tu Mwenyezi Mungu. Ghafla tu hivi litalia baragumu hilo la Kiama, vife dakika hiyo viumbe vyote, pasi na kuweza kuvuta khatwa moja kukimbilia nyumbani wala penginepo.

Basi yale Matangazo ya kuja Kiama anayonasibishiwa Sh. Ahmad mlinzi wa kaburi la Mtume, na ndoto hizo zinazotajwa humo, ni uwongo kabisa. Matangazo hayo yanatolewa na Mayahudi kutaka kuupa Uislamu jina baya ulimwenguni.

Kila Mwislamu akiipata karatasi hiyo NAAITIE MOTO AU NAAICHANECHANE Aitupe; siyo kuiandika chungu ya nakala na kuzitangaza. Ukifanya hivyo utakuwa unatangaza kutukanishwa Uislamu; basi utapata dhambi kubwa; siyo utapata thawabu kubwa kabisa kama inavyoandikwa humo.

Hapana faida ya kutaka kujua lini kitafika hicho Kiama. Kiama cha kila mtu ni siku ya kufa kwake. Na siku ya kufa kwake mtu pia haijui. Inataka kila wakati uwe umekwishatengeneza yako ya Akhera na unazidi kuongezea; na uwe umekwishategeneza yako ya Dunia, unazidi kuyaongezea kwani hujui yatatuwili vipi maisha yako. Basi tengenezea dunia yako kama kwamba utaishi sana, na tengenezea Akhera yako mbio mbio kama kwamba utakufa sasa hivi.

Mauti sidhani yana muhula — Milele ziumbe hufa ghafula

188. Makafiri wakimfanyia stihzai Mtume wakimwambia 'Tuangamize, basi Tufanyie hivi au Tuafanyie hivi kama kweli wewe ni Mtume.'

Basi ndiyo Mtume ameambiwa awajibu hapa kwamba hakuna Binaadamu yoyote anayeweza kujifanyia analolipenda au kuwafanyia wenziwe analolitaka, la nafuu wala 7la madhara. Wala hakuna anayejua ya ghaibu akapata kujivutia hili upesi au kujiepusha na hilo kwa haraka. Yote haya ni yake Mwenyewe Mwenyezi Mungu.

Na juu ya kuwa Mwenyezi Mungu amesema haya na akamwambia Mtume wake ajinasibishie haya; kuna watu wanaowaitakidia viumbe wenziwao uweza wa haya.

Uislamu namna huo una hatari. Si Uislamu huo. Kumuitakidia kiumbe mwenzio uweza wa Mwenyezi Mungu, na hali ya kuwa unamuona anataabishwa hata na kidudu chungu! Akili gani fupi hizo na itikadi gani potofu hizo!!

Anasema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 24 na 25 za *Suratun Najm* "Je! Mwanaadamu anaweza kupata kila anachotamani? Ni ya Mwenyezi Mungu tu Akhera na Dunia.

Na anasema mara nyingi kabisa kuwa Kujua Ghaibu kumo katika mikono ya Mwenyezi Mungu peke yake. Hakuna anayejua ya Ghaibu ila yeye 'Na huwapa baadhi ya Ghaibu hizo Mitume.'

Basi wasidanganywe watu, na wakakubali kudanganyika. Ya kufuatwa ni haya yanayosemwa katika Qurani na Hadithi Sahihi za Mtume; siyo ya kufuatwa hayo yanayopigiwa Ngoma tu na Watu.

189. Mwanamume wa kibinadamu na mwanamke wa kibinadamu wote wanatoka katika asili moja (nafsi moja), kwa Nabii Adamu na Bibi Hawwa. Na wote—hao wazee na kizazi—wameumbwa na Mwenyezi Mungu, na wanafanyiwa yote hayo na Mwenyezi Mungu. Ya kudhuru na ya kunufaisha. Yote yamo katika mikono ya Mwenyezi Mungu.

huwa wanamuomba Mwenyezi Mungu, Mola wao (wakisema): "Kama ukitupa (mtoto) mwema (kamili), tutakuwa miongoni mwa wanaoshukuru."

دَعَوَا اللّٰهَ رَبَّهُمَا لَئِنْ اٰتَيْتَنَا صَالِحًا لَّنَكُوْنَنَّ
مِنَ الشّٰكِرِيْنَ ﴿١٨٩﴾

190. Basi anapowapa (mtoto) mwema (kamili) wanamfanyia washirika Mungu katika kile alichowapa (Naye ni yule mtoto). Ametukuka Mwenyezi Mungu na huko kushirikisha kwao.

فَلَمَّآ اٰتٰىهُمَا صَالِحًا جَعَلَا لَهٗ شُرَكَآءَ فِيْمَآ
اٰتٰىهُمَا ۚ فَتَعٰلَى اللّٰهُ عَمَّا يُشْرِكُوْنَ ﴿١٩٠﴾

191. Wanawashirikisha (na Mungu) wale ambao hawaumbi kitu, hali wao wameumbwa?

192. Wala hawawezi kuwasaidia (hao wanaowaabudu), wala hawawezi kujisaidia (wenyewe) nafsi zao?

اَيُشْرِكُوْنَ مَا لَا يَخْلُقُ شَيْـًٔا وَّهُمْ يُخْلَقُوْنَ ﴿١٩١﴾
وَلَا يَسْتَطِيْعُوْنَ لَهُمْ نَصْرًا وَّلَآ اَنْفُسَهُمْ
يَنْصُرُوْنَ ﴿١٩٢﴾

193. Na kama (hao mnaowashirikisha na Mwenyezi Mungu) mkiwaita katika uwongofu hawatakufuateni (kwani hawasikii lolote wala hawatambui chochote). Ni mamoja kwenu ikiwa mtawaita au mtanyamaza kimya. (Hawana habari hawana lao jambo).

وَاِنْ تَدْعُوْهُمْ اِلَى الْهُدٰى لَا يَتَّبِعُوْكُمْ ۗ سَوَآءٌ
عَلَيْكُمْ اَدَعَوْتُمُوْهُمْ اَمْ اَنْتُمْ صَامِتُوْنَ ﴿١٩٣﴾

194. Hakika wale mnaowaabudu badala ya Mwenyezi Mungu ni waja (watumwa) kama nyinyi (bali nyinyi bora zaidi kuliko wao. Nyinyi mna midomo ya kusemea, wao hawana). Hebu waiteni, nao wakuitikieni, ikiwa mnasema kweli (kama wao ni bora na wanayo haya).

اِنَّ الَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِ اللّٰهِ عِبَادٌ
اَمْثَالُكُمْ فَادْعُوْهُمْ فَلْيَسْتَجِيْبُوْا لَكُمْ اِنْ كُنْتُمْ
صٰدِقِيْنَ ﴿١٩٤﴾

---

Na juu ya hivi binadamu hawasikii, tangu hao waliokuwa hawajapata Mitume na mpaka hao waliopata Mitume. Wote wamemtilia Mwenyezi Mungu ushirikina. Wameshishirikishia Mwenyezi Mungu Majina na wengineo kuwa wanaweza kudhuru wasipotiiwa, na wananufaisha wanapotiiwa na kuabudiwa. Basi kwa hivyo wale makafiri walipokuwa karibu ya kuzaa na wanaogopa nini litakuwa, walikuwa wakiweka nadhiri kuwa wakimzaa mtoto wao salama watamwita mtumwa wa huyo waliomshirikishia Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo waliita watoto wao. 'Mtumwa wa Jua.' Mtuwma wa huyo mungu wao wa sanamu waliokuwa wakimwita *Auf* au *Uzzaa* au *Manaa*.

Na Waislamu nao hawakusalimika na pepesi za ushirikina huu na mwingineo kama anavyosema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 106 ya *Surat Yusuf:* "Na wengi katika wao hawamuwamini Mwenyezi Muhgu isipokuwa na huku wanatia ushirikina."

Basi Waislamu hao kabla mtoto hajazaliwa—na wanaogopa asije akazaliwa amekufa au akazaliwa ameharibika—huweka nadhiri wakasema 'Nikizaa mtoto huyo nitamnyolea Sharifu Musa au kwa Hababa Amar au kwa Bi Kirembwe au kwa Mwana Mashungi au kwa Jundani au Mackinoni (Sharifu Aliyezikwa Mackinon Road) au . . .' Basi ndiyo hayo hayo yaliyokatazwa. Ati wanafanya hivi ili Sharifu Musa au Hababa au kwa Mwana Mashungi au Bi Kirembwe amhami huyo mtoto matumboni azaliwe kama anavyopenda na aishi.

Jambo gani linalowapelekea kufanya haya? Wanawaona hawa wanaweza kufanya asiyoyataka Mwenyezi Mungu? Au wanaona Mwenyezi Mungu hawasikii; yuko mbali nao; na hao ndio waliokaribu nao? Na hali ya kuwa Mwenyezi Mungu anawaambia katika Aya ya 186 ya *Surat Al-Baqarah* na Aya ya 16 ya *Surat Qaf* kuwa Wamuombe yeye tu na kuwa Yeye yuko karibu nao kweli kweli kuliko cho chote kile.

192. Masanamu yanaweza kujisaidia nini? Au mzimu unaweza kujisaidia nini? Au kaburi linaweza kujisaidia nini? Au . . . Yote haya yakifanyiwa lolote lile hayawezi kujipigania. Ndiyo wanatahayarishwa hawa wanaowacha kumuomba Mwenyezi Mungu wakamuomba asiyekuwa yeye.

195. (Nyinyi mna miguu ya kwendea). Je, wao wanayo miguu ya kwendea? Au wanayo mikono ya kushikia? Au wanayo macho ya kuonea? Au wanayo masikio ya kusikilizia? Sema: (Nabii Muhammad uwaambie washirikina hawa): "Waiteni hao mnaowashirikisha na Mungu, kisha nifanyieni kila vitimbi (vya kuniangamiza) wala msinipe nafasi yo yote (mara moja niangamizeni kama kweli wanaweza)."

اَلَهُمْ اَرْجُلٌ يَّمْشُوْنَ بِهَآ اَمْ لَهُمْ اَيْدٍ يَّبْطِشُوْنَ
بِهَآ اَمْ لَهُمْ اَعْيُنٌ يُّبْصِرُوْنَ بِهَآ اَمْ لَهُمْ
اٰذَانٌ يَّسْمَعُوْنَ بِهَا قُلِ ادْعُوْا شُرَكَآءَكُمْ
ثُمَّ كِيْدُوْنِ فَلَا تُنْظِرُوْنِ ﴿١٩٥﴾

196. Mlinzi wangu (wa kunihifadhi) ni Mwenyezi Mungu aliyeteremsha Kitabu (hiki kitukufu), naye ndiye awalindaye wafanyao mema (wote, si mimi tu).

اِنَّ وَلِيِّۦَ اللّٰهُ الَّذِيْ نَزَّلَ الْكِتٰبَ وَهُوَ يَتَوَلَّى
الصّٰلِحِيْنَ ﴿١٩٦﴾

197. Na wale mnaowaabudu badala yake hawana uweza wa kukunusuruni wala wa kujinusuru (wenyewe) nafsi zao.

وَالَّذِيْنَ تَدْعُوْنَ مِنْ دُوْنِهٖ لَا يَسْتَطِيْعُوْنَ
نَصْرَكُمْ وَلَآ اَنْفُسَهُمْ يَنْصُرُوْنَ ﴿١٩٧﴾

198. Na kama mkiwaita katika uwongofu hawasikii; na unawaona wanakutazama, lakini hawaoni. (Masanamu utayaona yamekodoa macho lakini kuona hapana).

وَاِنْ تَدْعُوْهُمْ اِلَى الْهُدٰى لَا يَسْمَعُوْا وَتَرٰىهُمْ
يَنْظُرُوْنَ اِلَيْكَ وَهُمْ لَا يُبْصِرُوْنَ ﴿١٩٨﴾

199. Shikamana na kusamehe na amrisha mema na wapuze masafihi.

خُذِ الْعَفْوَ وَاْمُرْ بِالْعُرْفِ وَاَعْرِضْ عَنِ
الْجٰهِلِيْنَ ﴿١٩٩﴾

200. Na kama wasiwasi wa Shetani ukikusumbua (kuona kwa nini nisiwajibu masafihi hawa) basi (sema *Audhu Billahi*) jikinge kwa Mwenyezi Mungu (na kuchezewa na Shetani, ukaacha wasia wake

وَاِمَّا يَنْزَغَنَّكَ مِنَ الشَّيْطٰنِ نَزْغٌ فَاسْتَعِذْ

---

195. Kila Mwislamu inataka awe na moyo mkubwa hivi. Akitishiwa kwa hiyo mizimu au masanamu au roho za wazee au . . . nawaambie 'Haya! Nawanidhuru nione.' Kila Mitume walipotishiwa walisema hivi. Na sisi tunaambiwa twende mwendo wao. Na tunaambiwa daima tuseme—kama ilivyo katika Aya ya 52 ya *Suratit Tawba* kuwa 'Halitatufika ila alilotuandikia Mwenyezi Mungu,' si lile wanalotutakia viumbe; na hali yakuwa Mwenyezi Mungu hakuliandika. Hilo halitufiki katu. Hata Shairi wa Kiswahili anasema:—

| | |
|---|---|
| Wakikushituwa | Wewe sishituke |
| Yupi awezaye | Kupitisha lake |
| Wakiwa na lao | Mungu ana Yake |
| Mambo yote ni ya Mungu | Atakalo ndilo huwa |
| Ndiye pweke Mwenye Quwa | Mwenye amri na shani |
| (Quwa | nguvu) |
| Kheri na sururu | Na wema uhai |
| Kipaji cha nuru | hakiniambai |
| Yao hayadhuru | wala hayafai |

Kuitakidi hivi ndio Uislamu. Sio kutetemeka kuogopa waganga na wachawi, na kuogopa mizimu na manazili mabaya au yaliyo kama haya.

199. Mtu hajibizani na wajinga. Mtu huwaonya tu mabaya na kuwaamrisha mema. Lakini maneno mabaya mtu hajibizani nao kwa mabaya. Ima Utawanyamazia au Utaondoka au Utawajibu kwa maneno ya kiakili kwa utaratibu na upole.

Utawafanyia haya masafihi unaokutana nao nje au ulio nao nyumbani; khasa wanawake, khasa mke.

200. Amebainisha Mwenyezi Mungu mara nyingi kuwa shetani ni adui yetu mkubwa kabisa, tumpige vita vikubwa, tusimkubalie kutushinda. Tuupige konde moyo, tusifuate anayoyataka. Basi hapa anatubainishia

Mwenyezi Mungu). Bila shaka Yeye ndiye asikiaye na ajuaye.

بِاللّٰهِ ۚ إِنَّهُ سَمِيعٌ عَلِيمٌ ﴿٢٠٠﴾

201. Wale wanaomuogopa (Mwenyezi Mungu) zinapowagusa pepesi za Shetani (wakaasi; kama hivyo kujibizana na masafihi) mara hukumbuka, tahamaki wamekwishaona njia.

إِنَّ الَّذِينَ اتَّقَوْا إِذَا مَسَّهُمْ طَيْفٌ مِّنَ الشَّيْطَٰنِ تَذَكَّرُوا فَإِذَا هُم مُّبْصِرُونَ ﴿٢٠١﴾

202. Na ndugu zao (wale walioasi pamoja nao) wanawavutia katika upotofu (upotevu) kisha wao hawaachi.

وَإِخْوَانُهُمْ يَمُدُّونَهُمْ فِي الْغَيِّ ثُمَّ لَا يُقْصِرُونَ ﴿٢٠٢﴾

203. Na usipowaletea Aya (wazitakazo) husema: "Kwa nini huzizui (mwenyewe)?" Sema: "Nayafuata yaliyofunuliwa kwangu (nilioletewa Wahyi) kutoka kwa Mola wangu (sizui mwenyewe). Hizi (Aya za Qurani) ni dalili (kubwa za ukweli wangu) zitokazo kwa Mola wenu na ni uwongofu na rehema kwa watu wanaoamini."

وَإِذَا لَمْ تَأْتِهِم بِآيَةٍ قَالُوا لَوْلَا اجْتَبَيْتَهَا ۚ قُلْ إِنَّمَا أَتَّبِعُ مَا يُوحَىٰ إِلَيَّ مِن رَّبِّي ۚ هَٰذَا بَصَائِرُ مِن رَّبِّكُمْ وَهُدًى وَرَحْمَةٌ لِّقَوْمٍ يُؤْمِنُونَ ﴿٢٠٣﴾

204. Na isomwapo Qurani isikilizeni na nyamazeni ili mpate kurehemewa.

وَإِذَا قُرِئَ الْقُرْآنُ فَاسْتَمِعُوا لَهُ وَأَنصِتُوا لَعَلَّكُمْ تُرْحَمُونَ ﴿٢٠٤﴾

205. Na mtaje Mola wako moyoni mwako kwa unyenyekevu na khofu na bila ya kupiga kelele katika kauli (yako hiyo usemi wako huo; mkumbuke Mola wako umtaje) asubuhi na jioni; wala usiwe miongoni mwa walioghafilika.

وَاذْكُر رَّبَّكَ فِي نَفْسِكَ تَضَرُّعًا وَخِيفَةً وَدُونَ الْجَهْرِ مِنَ الْقَوْلِ بِالْغُدُوِّ وَالْآصَالِ وَلَا تَكُن مِّنَ الْغَافِلِينَ ﴿٢٠٥﴾

---

Mwenyezi Mungu kuwa natumtake vile vile Mwenyezi Mungu atusaidie kumshinda huyo shetani kama vile kusema *Audhu Billahi Minah Shaytanir Rajym*, ukihisi kukushawishi kwake.

201. Kuonyesha kuwa hata hao wenye kumcha Mwenyezi Mungu hutokea wakatelezeshwa na Shetani wakaasi kidogo; lakini mara hutanabahi wakarejea kwa Mwenyezi Mungu, na Mwenyezi Mungu akawasamehe.

Binaadamu ni mahala pake kukosa wakati mwengine—Akaacha kulitenda aliloambiwa kulitenda au akafanya aliloambiwa kuliacha.

Basi wale Waislamu wema mara tu wakijiona wameteleza wamepotea njia, mara huacha ile njia waliopotelea, wakashika ile yao nzuri ya asili.

202. Mwema hapotei ila kwa mbaya. Na kama watu wema wanavyowavutia watu kwenda katika wema, wakahuzunika wanapowatoka, wakaingia kuwavuta tena; ndivyo wabaya nao walivyo. Wanaweta watu katika ubaya. Wakiwapata wakafurahi; wakiwatoka wakahuzunika na, wakajitahidi kuwavuta tena.

203. Yale Makafiri makubwa yalikuwa yakiwaudhi kweli kweli yale mambo aliyokuja nayo Nabii Muhammad ya kulazimisha kutekeleza haki, kufanya mema, kuweka usawa, kuwapa msaada masikini na kuwanyanyua, na yaliyo kama haya.

Basi wakimwambia Mtume kuwa 'Ukitaka tukufuate tuletee kinyume cha mambo haya.' Mtume huwaambia 'Mimi ninaletewa Aya namna hizi.' Basi humwambia 'Zua zako mwenyewe zifuate hivyo tunavyotaka sisi.'

204. Kama ilivyokupasa kuihishmu Qurani kwa kufuata maamrisho yake na kuyaepuka makatazo yake; na vile vile inastahiki kutukuzwa kwa matukuzo mengine, kama kunyamaza kimya inaposomwa, kuikamata kwa hishima, kuiweka mahala pa hishima, kuisoma kwa hishima na kama haya.

205. Waislamu wanahimizwa daima kumuona Mwenyezi Mungu mbele ya macho yao; na wawe wanamtaja mara kwa mara kwa nyoyo zao na ndimi zao; kwa kusoma Qurani na kwa kusoma nyuradi na yaliyo kama haya. Lakini ikiwa moyoni tu hivi au kwa sauti ndogo tu bila ya kelele, ndio bora; ingawa kwa sauti zisizokuwa kubwa

206. Wale walioko kwa Mola wako (Nao ni Malaika) hawajivuni (wakaacha) kumuabudu (Mola wao kwa kuwa ni wakubwa la; bali) na wanamtukuza na kumsujudia.

إِنَّ الَّذِينَ عِندَ رَبِّكَ لَا يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ
عِبَادَتِهِ وَيُسَبِّحُونَهُ وَلَهُ يَسْجُدُونَ ۩ ﴿٢٠٦﴾

---

sana inakubalishwa, lakini bora zaidi kwa sauti ndogo. Na watu wote takriba wanafanya kinyume cha haya. Hata mazikoni—mahala pa kumkumbuka Mwenyezi Mungu kweli kweli—na Mtume ametuamrisha tusinyanyue sauti ila sauti ndogo kabisa ya kujisikia mtu mwenyewe tu au tumtaje moyoni tu basi. Amesema Mtume: "Jeneza halifuatwi kwa sauti yo yote ile . . .'

206. Unapomaliza kusoma Aya hii ya 206 na ikawa una udhu, imesuniwa Usujudu Sijida moja—kuwiga hicho kitendo cha Malaika wanachokifanya cha kumsujudia Mwenyezi Mungu.

Utakaa uelekee Kibla (Kwa Kiibadhi si lazima kuelekea kibla); utie nia kuwa unasujudu sijida ya kusoma Qurani. Useme *Allahu Akbar* Mara Usujudu ulete zile zile *Subhana* za Sijida. Uinuke, Utoe salamu (Hapana Tahiyatu wala cho chote). Na sijda yenyewe ni moja tu, si mbili kama dasturi ya sijda.

Na unaweza kuleta dua katika ile sijda baada ya kwisha kusoma zile *Subhana*. Moja katika dua hizo ni kusema kwa Kiarabu, 'Ee Mola wangu! Kwa sijda hii niangushie madhambi yangu. Na kwa sijda hii niandikie thawabu nyingi. Na uifanye sijda hii ni akiba yangu ninayoiweka huko kwako inifae siku ya Kiama.'

Bali hata akiwamo ndani ya sala atateremka asujudu, arejee katika kisimamo kutimiza sala yake.

اٰياتها ٧٥ (٨) سُوْرَةُ الْاَنْفَالِ مَدَنِيَّةٌ (٨٨) رُكوعاتها ١٠

Ina Aya 75

# SURATUL ANFAL

*(Imeteremka Madina)*

Ina Makara 10

بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ

Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwenye kuneemesha neema kubwa kubwa na Mwenye kuneemesha neema ndogo ndogo.

يَسْـَٔلُوْنَكَ عَنِ الْاَنْفَالِ ۭ قُلِ الْاَنْفَالُ لِلّٰهِ وَالرَّسُوْلِ ۚ فَاتَّقُوا اللّٰهَ وَاَصْلِحُوْا ذَاتَ بَيْنِكُمْ ۠ وَاَطِيْعُوا اللّٰهَ وَرَسُوْلَهٗٓ اِنْ كُنْتُمْ مُّؤْمِنِيْنَ ①

1. Wanakuuliza juu ya mali yaliyotekwa (ngawira; yagaiwe vipi?) Sema: "Mali yaliyotekwa ni ya Mwenyezi Mungu na Mtume, (fuateni watakavyokugawieni). Basi muogopeni Mwenyezi Mungu na suluhisheni mambo baina yenu, na mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake ikiwa nyinyi ni katika wanaoamini (kweli)."

اِنَّمَا الْمُؤْمِنُوْنَ الَّذِيْنَ اِذَا ذُكِرَ اللّٰهُ وَجِلَتْ قُلُوْبُهُمْ وَاِذَا تُلِيَتْ عَلَيْهِمْ اٰيٰتُهٗ زَادَتْهُمْ اِيْمَانًا وَّعَلٰي رَبِّهِمْ يَتَوَكَّلُوْنَ ②

2. Hakika wanaoamini kweli ni wale ambao anapotajwa Mwenyezi Mungu nyoyo zao hujaa khofu; na wanaposomewa Aya zake huwazidishia imani, na wakamtegemea Mola wao tu basi; (hawana kuamini mizimu wala pango wala shetani wala makaburi wala mengineyo).

الَّذِيْنَ يُقِيْمُوْنَ الصَّلٰوةَ وَمِمَّا رَزَقْنٰهُمْ يُنْفِقُوْنَ ③

3. Ambao wanasimamisha Sala na wanatoa katika yale tuliyowapa.

اُولٰۗىِٕكَ هُمُ الْمُؤْمِنُوْنَ حَقًّا ۭ لَهُمْ دَرَجٰتٌ عِنْدَ رَبِّهِمْ وَمَغْفِرَةٌ وَّرِزْقٌ كَرِيْمٌ ④

4. Hao ndio wanaoamini kweli kweli. Wao wana vyeo (vikubwa) kwa Mola wao, na msamaha na riziki bora (kabisa huko Akhera).

كَمَآ اَخْرَجَكَ رَبُّكَ مِنْۢ بَيْتِكَ بِالْحَقِّ ۠ وَاِنَّ فَرِيْقًا مِّنَ الْمُؤْمِنِيْنَ لَكٰرِهُوْنَ ⑤

5. (Atakunusuru) kama alivyokutoa Mola wako katika nyumba yako kwa haki, na kundi moja la walioamini halipendi (utoke)

---

1. Yaani Sura ya kutaja namna ya kugawa ngawira (nyara) inayopatikana katika vita.

Waislamu walipokuwa Makka walikuwa wakionewa na kudhulumiwa bali na kuuawa kwa namna mbaya mbaya za kuuawa. Baada ya miaka kumi na mitatu ya taabu hii walihamia Madina ili wakapate salama. Lakini haikupatikana. Wale Maqureshi na Makafiri wengine walikuwa wanawendea na kutia moto mitende yao na kuchukua wanyama wao bali na kuteka na kuua baadhi ya watu wanaowapatia wasaa—wanaume na wanawake. Na hao waliokuwa wakiwateka, wakenda nao kwao wakiwaua kwa shangwe kubwa na furaha au huwauza miji mingine au huwaweka majumbani mwao kuwatumia na kuwatumikia.

Mambo yalipotopea hivi Mwenyezi Mungu aliwapa ruhusa Waislamu nao wakipigwa, wachukue nao wakichukuliwa. Akasema Mwenyezi Mungu katika Aya ya 39 ya *Suratul Haj* "Wameruhusiwa (kupigana) wale wanaopigwa, kwa sababu wamedhulumiwa."

Basi katika mwaka wa pili wa Al Hijra wakatiana mkononi Waislamu na makafiri katika uwanja wa Badri—baina ya Makka na Madina. Waislamu walikuwa mia tatu sabi-in na kitu, na makafiri wakawa elfu na kitu. Na juu ya hivi Waislamu wakashinda, wakapata ngawira nyingi na mateka sabi-ini nawakaua wakubwa wa Kiqureshi sabi—ini.

Basi katika Sura hii inatajwa kidogo habari hiyo na namna ya kugawa kila ngawira watakayoipata; usiwepo mgogoro tena kama uliotaka kutokea hapo walipotaka kugawa hiyo ngawira.

2. Hapa zinatajwa baadhi ya sifa za Waislamu wa kweli. Asiyekuwa nazo basi anajigamba tu. Na kujigamba hakuna maana.

5. Ilipoadia kutaka kwenda kukabiliana kwa vita na Maqureshi, baadhi ya Waislamu waliogopa kwani ndio

6. Wakabishana nawe katika (lile jambo la) haki baada ya kubainika (haki ile; wanachukiwa kwenda huko vitani) kama kwamba wanasukumwa katika mauti na huku wanaona.

يُجَادِلُونَكَ فِي الْحَقِّ بَعْدَمَا تَبَيَّنَ كَأَنَّمَا
يُسَاقُونَ إِلَى الْمَوْتِ وَهُمْ يَنظُرُونَ ﴿٦﴾

7. Na (kumbukeni) Mwenyezi Mungu alipokuahidini moja katika mataifa mawili ya kwamba ni lenu. Nanyi mkapenda mupate lile lisilo na nguvu; na Mwenyezi Mungu anapenda kuthubutisha haki kwa maneno yake na (anapenda) kuikata mizizi ya makafiri

وَإِذْ يَعِدُكُمُ اللَّهُ إِحْدَى الطَّائِفَتَيْنِ أَنَّهَا
لَكُمْ وَتَوَدُّونَ أَنَّ غَيْرَ ذَاتِ الشَّوْكَةِ تَكُونُ
لَكُمْ وَيُرِيدُ اللَّهُ أَن يُحِقَّ الْحَقَّ بِكَلِمَاتِهِ
وَيَقْطَعَ دَابِرَ الْكَافِرِينَ ﴿٧﴾

8. Ili kuthubutisha haki na kuiondoa batili; hata wakichukia watu wabaya.

لِيُحِقَّ الْحَقَّ وَيُبْطِلَ الْبَاطِلَ وَلَوْ كَرِهَ الْمُجْرِمُونَ ﴿٨﴾

9. (Kumbukeni) mlipokuwa mkiomba msaada kwa Mola wenu, naye akakujibuni kuwa: "Kwa yakini Mimi nitakusaidieni kwa Malaika elfu moja watakaofuatana mfululizo (wanaongezeka tu)."

إِذْ تَسْتَغِيثُونَ رَبَّكُمْ فَاسْتَجَابَ لَكُمْ أَنِّي
مُمِدُّكُم بِأَلْفٍ مِّنَ الْمَلَائِكَةِ مُرْدِفِينَ ﴿٩﴾

10. Na Mwenyezi Mungu hakufanya haya ila iwe bishara (habari ya furaha) na ili nyoyo zenu zitue kwayo. Na hakuna msaada (wa kufaa) ila utokao kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

وَمَا جَعَلَهُ اللَّهُ إِلَّا بُشْرَىٰ وَلِتَطْمَئِنَّ بِهِ
قُلُوبُكُمْ ۚ وَمَا النَّصْرُ إِلَّا مِنْ عِندِ اللَّهِ ۚ ع ١٥
إِنَّ اللَّهَ عَزِيزٌ حَكِيمٌ ﴿١٠﴾

11. (Kumbukeni) alipokuleteeni usingizi uliokuwa (alama ya) salama itokayo kwake, na akakuteremshieni maji mawinguni ili kukutahirisheni kwayo na kukuondoleeni uchafu wa Shetani na

إِذْ يُغَشِّيكُمُ النُّعَاسَ أَمَنَةً مِّنْهُ وَيُنَزِّلُ
عَلَيْكُم مِّنَ السَّمَاءِ مَاءً لِّيُطَهِّرَكُم بِهِ
وَيُذْهِبَ عَنكُمْ رِجْزَ الشَّيْطَانِ وَلِيَرْبِطَ عَلَىٰ

---

mara yao ya awali kutaka kukabiliana nao, na hali ya kuwa hao Maqureshi ni mashujaa na wana silaha kamili na ni wengi sana kabisa kuliko wao. Basi wakitoa udhuru huu na udhuru huu.

7. Ilipokuja ile amri ya kukabiliana na Maqureshi ilikuwa ima walikabili jeshi lao Maqureshi lililokuwa limezatiti barabara, au waukabili msafara wao wa watu 40 tu na uliokuwa na mali kubwa, na wao Waislamu walikuwa watu mia tatu. Na walipewa ahadi na Mwenyezi Mungu kuwa lo lote watakalolifuata watashinda wao Waislamu. Wakilifuata hilo jeshi kubwa la Maqureshi watalishinda; na wakiufuata huo msafara mdogo wenye mali pia watawashinda. Waislamu wengi—kwa vile wana woga — walipenda waufuate ule msafara wajiepushe na lile jeshi. Lakini Mwenyezi Mungu alikuwa anataka wakabiliane na hilo la Maqureshi. Basi likafuatwa Shauri la kupigana. Na kwa rehema za Mwenyezi Mungu Waislamu wakashinda.

9. Walipokuja Waislamu wakakutana na jeshi la Kiqureshi kubwa lile, waliogopa sana, wakaingia kumwomba Mwenyezi Mungu kwa dhati yao awape nusura juu ya dini yao.

Na Mwenyezi Mungu akatoa waadi huu kumpa Mtume kuwa watakuja Malaika kwa sura ya Kibinadamu, wawe pamoja na Waislamu; ima wapigane khasa kwa nguvu za Kibinadamu au waongezee tu lile jeshi, lionekane kubwa, zitue nyoyo za Waislamu na zipapatike nyoyo za makafiri.

10-11. Baada ya kupata ahadi ile kwa Mwenyezi Mungu kuwa wakati wa vita atawaletea Malaika, basi Waislamu walitua nyoyo zao, wakapata usingizi mzuri na kulala; hata wengine wakaota, wakajiharibu, ikawapasa waoge, na maji hapana. Mara mvua ikanya; wakapata maji ya kuogea na ya kutumia kwa haja nyingine. Na uwanja ule wa Badri ulikuwa una mchanga namna mbili, Mchanga wa upande mmoja ulikuwa haujishiki kabisa

قُلُوبِكُمْ وَيُثَبِّتَ بِهِ الْأَقْدَامَ ﴿١١﴾

kuzipa nguvu nyoyo zenu na kuithubutisha miguu yenu chini (isiwe inazamazama mchangani).

إِذْ يُوحِي رَبُّكَ إِلَى الْمَلَائِكَةِ أَنِّي مَعَكُمْ
فَثَبِّتُوا الَّذِينَ آمَنُوا ۚ سَأُلْقِي فِي قُلُوبِ
الَّذِينَ كَفَرُوا الرُّعْبَ فَاضْرِبُوا فَوْقَ
الْأَعْنَاقِ وَاضْرِبُوا مِنْهُمْ كُلَّ بَنَانٍ ﴿١٢﴾

12. (Kumbukeni) Mola wako alipowafunulia Malaika (akawaambia): "Hakika Mimi ni pamoja nanyi, basi watieni nguvu wale walioamini; nitatia woga katika nyoyo za makafiri. Basi wapigeni juu ya shingo (zao) na kateni kila ncha za vidole vyao.

ذَٰلِكَ بِأَنَّهُمْ شَاقُّوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ ۚ وَمَن
يُشَاقِقِ اللَّهَ وَرَسُولَهُ فَإِنَّ اللَّهَ شَدِيدُ
الْعِقَابِ ﴿١٣﴾

13. Hayo ni kwa sababu wamemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake. Na mwenye kumuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake (atamuadhibisha) kwani Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

ذَٰلِكُمْ فَذُوقُوهُ وَأَنَّ لِلْكَافِرِينَ
عَذَابَ النَّارِ ﴿١٤﴾

14. (Hiyo ni adhabu ya Mwenyezi Mungu, enyi Maqureshi!) Basi ionjeni (ya kuuawa hivyo na kutekwa hivyo). Na bila shaka makafiri wana adhabu (nyingine) na moto (inawangojea Akhera).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا لَقِيتُمُ الَّذِينَ
كَفَرُوا زَحْفًا فَلَا تُوَلُّوهُمُ الْأَدْبَارَ ﴿١٥﴾

15. Enyi Mlioamini! Mkutanapo vitani na wale waliokufuru basi msiwageuzie migongo (mkakimbia).

وَمَن يُوَلِّهِمْ يَوْمَئِذٍ دُبُرَهُ إِلَّا مُتَحَرِّفًا
لِّقِتَالٍ أَوْ مُتَحَيِّزًا إِلَىٰ فِئَةٍ فَقَدْ بَاءَ بِغَضَبٍ
مِّنَ اللَّهِ وَمَأْوَاهُ جَهَنَّمُ ۖ وَبِئْسَ الْمَصِيرُ ﴿١٦﴾

16. Na atakayewageuzia mgongo wake siku hiyo—isipokuwa amegeuka kwa kushambulia au amegeuka akaungane na sehemu nyingine za jeshi hili hili la Waislamu—(ikiwa si hivyo) atastahiki ghadhabu ya Mwenyezi Mungu; na mahali pake ni Jahanamu. Napo ni mahali pabaya pa kurudia (mtu).

فَلَمْ تَقْتُلُوهُمْ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ قَتَلَهُمْ ۚ وَمَا
رَمَيْتَ إِذْ رَمَيْتَ وَلَٰكِنَّ اللَّهَ رَمَىٰ ۚ وَلِيُبْلِيَ
الْمُؤْمِنِينَ مِنْهُ بَلَاءً حَسَنًا ۚ إِنَّ اللَّهَ سَمِيعٌ
عَلِيمٌ ﴿١٧﴾

17. Hamkuwaua nyinyi lakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyewaua; na hukutupa wewe (Mtume ule mchanga wa katika gao la mkono wako), ulipotupa (ukawaingia wote machoni mwao); (hukufanya wewe haya) walakini Mwenyezi Mungu ndiye aliyeutupa, (yaani ndiye aliyeufikisha katika macho yao wote yakawa yanawawasha kuliko pilipili, wakenda mbio) Alifanya haya Mwenyezi Mungu ili awape walioamini hidaya nzuri itokayo kwake. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye.

ذَٰلِكُمْ وَأَنَّ اللَّهَ مُوهِنُ كَيْدِ الْكَافِرِينَ ﴿١٨﴾

18. Basi haya (mumefanyiwa safari hii). Na hakika Mwenyezi Mungu atazidhoofisha nguvu za makafiri (atazivunja).

---

unatumbukiza miguu. Nao ndio ule wa upande walioko Waislamu. Basi ilipokunya ile mvua mchanga ule ulipata maji ukawa wa kujishika barabara. Wakastarehe Waislamu. Ukaharibika mchanga wa upande wa Maqureshi, ikawa matope na kunyekenya.

12. Katika namna za kutiwa moyo hao Waislamu wazuri.

15. Wanahimizwa wawe wanaume barabara.

17. Vita viliposhtadi Mtume alichukua gao la mchanga akalitia kiganjani akausomea na kuomba dua. Kisha akalivurumiza katika hilo jeshi la maadui; ukaingia mchanga huo katika jicho la kila mmoja katika hao.

إِن تَسْتَفْتِحُوا فَقَدْ جَاءَكُمُ الْفَتْحُ ۖ وَإِن تَنتَهُوا
فَهُوَ خَيْرٌ لَّكُمْ ۖ وَإِن تَعُودُوا نَعُدْ وَلَن تُغْنِيَ
عَنكُمْ فِئَتُكُمْ شَيْئًا وَلَوْ كَثُرَتْ وَ
أَنَّ اللَّهَ مَعَ الْمُؤْمِنِينَ ﴿١٩﴾

19. Kama (nyinyi Maqureshi) mnataka hukumu (ya kupambanua baina ya haki na batili) basi hukumu imekwisha kufikieni (mumeona .kuwa nyinyi ndio mlio katika batili. Mumeshindwa na chembe ya watu). Na kama mkijizuia (na kupigana na Waislamu) basi itakuwa bora kwenu. Na kama mtarudia (kupigana nao) Sisi pia tutarudia (kuwatia nguvu wakushindeni). Na watu wenu hawatakufaeni cho chote hata wakiwa wengi. Na Mwenyezi Mungu yu pamoja na wanaoamini.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَرَسُولَهُ
وَلَا تَوَلَّوْا عَنْهُ وَأَنتُمْ تَسْمَعُونَ ﴿٢٠﴾

20. Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na Mtume wake, wala msijiepushe naye na hali mnasikia.

وَلَا تَكُونُوا كَالَّذِينَ قَالُوا سَمِعْنَا وَهُمْ
لَا يَسْمَعُونَ ﴿٢١﴾

21. Wala msiwe kama wale wanaosema: "Tumesikia (tumetii)," na kumbe hawasikii (hawatii lo lote).

إِنَّ شَرَّ الدَّوَابِّ عِندَ اللَّهِ الصُّمُّ الْبُكْمُ الَّذِينَ
لَا يَعْقِلُونَ ﴿٢٢﴾

22. Hakika vinyama viovu mbele ya Mwenyezi Mungu ni hawa wanaojipa uziwi (wa kutosikia haki), wanaojipa ububu (wasiikiri hiyo haki), ambao hawayatii akilini (wanayoambiwa, bali wanayakataa tu vivi hivi bila ya kuyapima kwanza).

وَلَوْ عَلِمَ اللَّهُ فِيهِمْ خَيْرًا لَّأَسْمَعَهُمْ ۖ وَلَوْ أَسْمَعَهُمْ
لَتَوَلَّوا وَّهُم مُّعْرِضُونَ ﴿٢٣﴾

23. Na kama Mwenyezi Mungu angalijua wema wo wote kwao, angewasikilizisha; na kama angeliwasikilizisha wangeligeuka (vile vile) wakapuza.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا اسْتَجِيبُوا لِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ إِذَا
دَعَاكُمْ لِمَا يُحْيِيكُمْ ۖ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ يَحُولُ
بَيْنَ الْمَرْءِ وَقَلْبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيْهِ تُحْشَرُونَ ﴿٢٤﴾

24. Enyi mlioamini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume wake anapokuiteni katika yale yatakayokupeni uhai mzuri (wa duniani na Akhera. Fuateni amri zake Mwenyezi Mungu na makatazo yake). Na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake (mara akafa. Basi asiakhirisheakhirishe kwa kutumaini uhai; na jueni), kuwa kwake Yeye mtakusanywa (mulipwe kwa kila mlilolifanya).

وَاتَّقُوا فِتْنَةً لَّا تُصِيبَنَّ الَّذِينَ ظَلَمُوا مِنكُمْ
خَاصَّةً ۖ وَاعْلَمُوا أَنَّ اللَّهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ ﴿٢٥﴾

25. Na iogopeni adhabu ya (Mwenyezi Mungu ya hapa duniani) ambayo haitawasibu peke yao wale waliodhulumu nafsi zao miongoni mwenu (bali itawasibu hata walionyamaza wasiwakataze, bali na wengineo pia); na jueni ya kuwa Mwenyezi Mungu ni mkali wa kuadhibu.

---

*N.B.*—Siku ya vita vya Badri Makafiri walikuwa wengi sana kuliko Waislamu. Na juu ya hivi Waislamu waliwashinda; waliwaua wengi na wakawateka wengi. Basi Mwenyezi Mungu anawaambia hivi.

20-23. Anataja Mwenyezi Mungu ubaya wa wanaosikia ya kheri wasiyafuate. Kuwa ni watu wabaya kabisa.

24. Wanafahamishwa viumbe wote kuwa kila analowaitia Mtume ni la kheri yao viumbe vyote duniani na Akhera. Na wanafahamishwa nguvu za Mwenyezi Mungu kuwa anaweza kufanya atakavyo; na juu ya hivi hawafanyii waja Wake ila ya kheri tu.

Makadiyani katika maelezo ya hii Aya waliyoita ya 25 wanawaziba watu macho na kuwababaisha wasadiki uwongo wao wa kukataa miujiza aliyoitaja Mwenyezi Mungu ya kufufuliwa baadhi ya waliokufa. Na tumeitaja

26. Na kumbukeni (enyi Waislamu) mlipokuwa wachache, mkionekana madhaifu katika ardhi; mkawa mnaogopa watu wasikunyakueni (kukuibeni); akakupeni mahala pazuri pa kukaa (Napo ni hapa Madina) na akakutieni nguvu kwa nusura yake, na akakupeni riziki nzuri ili mupate kushukuru.

وَاذْكُرُوا إِذْ أَنتُمْ قَلِيلٌ مُّسْتَضْعَفُونَ
فِي الْأَرْضِ تَخَافُونَ أَن يَتَخَطَّفَكُمُ النَّاسُ
فَآوَاكُمْ وَأَيَّدَكُم بِنَصْرِهِ وَرَزَقَكُم مِّنَ الطَّيِّبَاتِ
لَعَلَّكُمْ تَشْكُرُونَ ﴿٢٦﴾

27. Enyi mlioamini! Msimfanyie khiana Mwenyezi Mungu na Mtume (mkaacha kufuata mlioamrishwa) wala msikhini amana zenu (mnazoaminiana wenyewe kwa wenyewe); na hali mnajua (kuwa ni vibaya hivyo).

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَخُونُوا اللَّهَ وَالرَّسُولَ وَ
تَخُونُوا أَمَانَاتِكُمْ وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٧﴾

28. Na jueni ya kwamba mali zenu na watoto wenu ni mtihani (huo aliokupeni Mwenyezi Mungu kutazama mtaendesha vipi) na jueni ya kwamba kwa Mwenyezi Mungu yako malipo makuu (kabisa).

وَاعْلَمُوا أَنَّمَا أَمْوَالُكُمْ وَأَوْلَادُكُمْ فِتْنَةٌ
وَأَنَّ اللَّهَ عِندَهُ أَجْرٌ عَظِيمٌ ﴿٢٨﴾ ع

29. Enyi mlioamini! Mkimcha Mwenyezi Mungu atakupeni tamyizi ya kupambanua baina ya haki na batili na atakufutieni makosa yenu na kukusameheni. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye fadhila kubwa kabisa.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِن تَتَّقُوا اللَّهَ يَجْعَل لَّكُمْ
فُرْقَانًا وَيُكَفِّرْ عَنكُمْ سَيِّئَاتِكُمْ وَيَغْفِرْ لَكُمْ ۗ وَاللَّهُ
ذُو الْفَضْلِ الْعَظِيمِ ﴿٢٩﴾

30. Na (kumbuka Ee Nabii Muhammad) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge au wakuue au wakutoe (kwa hali mbaya katika Makka); na wakafanya hila (zao barabara); Na Mwenyezi Mungu akazipindua hila hizo. Na Mwenyezi Mungu ni mbora wa kupindua hila (za watu wabaya).

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ
أَوْ يُخْرِجُوكَ ۚ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۖ وَاللَّهُ
خَيْرُ الْمَاكِرِينَ ﴿٣٠﴾

31. Na (Maqureshi) wanaposomewa Aya zetu, husema: "Tumekwishasikia (hayo zamani). Na lau

وَإِذَا تُتْلَىٰ عَلَيْهِمْ آيَاتُنَا قَالُوا قَدْ سَمِعْنَا
لَوْ نَشَاءُ لَقُلْنَا مِثْلَ هَٰذَا ۙ إِنْ هَٰذَا إِلَّا

---

habari hii katika Marejezo ya maelezo ya Aya ya 56 ya *Suratul Baqarah*.

25. Watu wema wanaambiwa wasiwaachie watu waovu kufanya maovu yao bila ya kuwakataza kwani adhabu ya duniani ikija itawachukua wema na wabaya, khalafu hao wema waipate salama ya huko, lakini balaa ya huku imewafika. Balaa kubwa — kama rehema kubwa — inaenea kwa wote.

26. Watu wanapokuwa katika neema inataka wakumbuke hali mbaya waliyokuwa nayo, wazidi kushukuru neema iliyowafikia na waondoshe maasi kwani hapana linaloondosha neema kama maasi na kutoishukuru hiyo neema.

28. Watu wengi wanaiba na kunyang'anya na kudhulumu na kufanya mengineyo yasiyo njia kwa sababu ya kutaka kupata mali wao na kuwatononesha watoto wao. Basi yasiwe hayo. Watajikosesha thawabu za Mwenyezi Mungu. Watajikosesha wingi kwa uchache. Na kuna jukumu kubwa kwa wazee juu ya watoto wao. Lazima juu yao wawatengezee dini yao na dunia yao; na mali lazima yatolewe mazakaa na yatumiwe katika njia nyingine za kheri. Basi mtihani mkubwa, si neema tupu hiyo.

29. Mtu akimcha Mwenyezi Mungu atafungukiwa duniani na Akhera.

30. Hapa inatajwa ile mikutano yao Maqureshi waliyoifanya Makka kabla Mtume hajaondoka. Walikutanika katika jumba lao la mikutano huko wakatoa shauri kutafuta lipi la kumfanyia Nabii Muhammad limuangamize.

Wengine walisema afungwe huko Makka bila ya kupewa chakula—au kwa kupewa chakula kidogo kabisa—mpaka afe. Wengine wakasema azibwe macho, azibwe mdomo, atiwe pingu za mikono na miguu, apandishwe juu ya ngamia aliyetiwa vitunga vya macho, akatupwe majangwani huko, ahangaike mpaka afe kwa kiu na njaa na jua.

tungependa tungesema kama haya. Haya si cho chote ila ni hadithi tu za watu wa kale."

أَسَاطِيرُ الْأَوَّلِينَ ﴿٣١﴾

32. Na (kumbuka) waliposema (makafiri): "Ee Mwenyezi Mungu! Kama haya (aliyokuja nayo Muhammad) ni haki itokayo kwako, basi tupige kwa mvua ya mawe yanayotoka mbinguni au tuletee adhabu nyingine iumizayo (yoyote ile; lakini sisi hatufuati)."

وَإِذْ قَالُوا اللَّهُمَّ إِن كَانَ هَٰذَا هُوَ الْحَقَّ
مِنْ عِندِكَ فَأَمْطِرْ عَلَيْنَا حِجَارَةً مِّنَ السَّمَاءِ
أَوِ ائْتِنَا بِعَذَابٍ أَلِيمٍ ﴿٣٢﴾

33. Lakini Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu maadamu wewe (Nabii Muhammad) umo pamoja nao (hapa Makka), wala Mwenyezi Mungu hakuwa wa kuwaadhibu pia hali ya kuwa (baadhi yao wamesilimu) wanaomba msamaha.

وَمَا كَانَ اللَّهُ لِيُعَذِّبَهُمْ وَأَنتَ فِيهِمْ ۚ وَمَا كَانَ
اللَّهُ مُعَذِّبَهُمْ وَهُمْ يَسْتَغْفِرُونَ ﴿٣٣﴾

34. Lakini wao (Makureshi) wana jambo gani (zuri) hata Mwenyezi Mungu asiwaadhibu; na hali ya kuwa wanawazuilia (watu) na huo Msikiti Mtakatifu? Nao hawakuwa walinzi wake (msikiti huo). Hawakuwa walinzi wake (na walinzi wa kila msikiti) isipokuwa wacha Mungu tu, lakini wengi katika wao hawajui lolote, (wanajisemea tu).

وَمَا لَهُمْ أَلَّا يُعَذِّبَهُمُ اللَّهُ وَهُمْ يَصُدُّونَ عَنِ
الْمَسْجِدِ الْحَرَامِ وَمَا كَانُوا أَوْلِيَاءَهُ ۚ
إِنْ أَوْلِيَاؤُهُ إِلَّا الْمُتَّقُونَ وَلَٰكِنَّ أَكْثَرَهُمْ
لَا يَعْلَمُونَ ﴿٣٤﴾

35. Na haikuwa ibada yao (hao makafiri) hapo katika hiyo nyumba tukufu ila kupiga miunzi (mbinja) na kupiga kofi. Basi (wataambiwa) onjeni adhabu (leo) kwa sababu ya kule kukufuru kwenu."

وَمَا كَانَ صَلَاتُهُمْ عِندَ الْبَيْتِ إِلَّا مُكَاءً
وَتَصْدِيَةً ۚ فَذُوقُوا الْعَذَابَ بِمَا كُنتُمْ
تَكْفُرُونَ ﴿٣٥﴾

36. Hakika wale waliokufuru hutoa mali zao ili kuzuilia (watu wasipate kuamini) njia ya Mwenyezi Mungu. Basi watazitoa, kisha zitakuwa majuto juu yao, kisha watashindwa. Na wale waliodumu katika ukafiri watakusanywa katika Jahanamu (Watakaosilimu baadaye Mungu atawasamehe).

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا يُنفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ
لِيَصُدُّوا عَن سَبِيلِ اللَّهِ ۚ فَسَيُنفِقُونَهَا
ثُمَّ تَكُونُ عَلَيْهِمْ حَسْرَةً ثُمَّ يُغْلَبُونَ ۗ
وَالَّذِينَ كَفَرُوا إِلَىٰ جَهَنَّمَ يُحْشَرُونَ ﴿٣٦﴾

---

Wengine wakasema wachaguliwe vijana watukufu wamshambulie mara moja wote na kumua. Na hii sehemu ya mwisho ndiyo iliyokubaliwa. Lakini usiku ule Mtume alihama kwenda Madina, wasiwahi lo lote.

31. Waongo Maqureshi, wanajitia pambani tu. Ndio silaha ya mwenye kushindwa, huko kutukana. Mara ngapi wameambiwa katika Qurani walete maneno kama haya ya Qurani japo kijisura kimoja kifupi tu. Nao walishindwa kabisa kabisa. Na huku nyuma hujidai kuwa wanaweza. Basi kwa nini hawafanyi kama wanaweza? Waliambiwa katika Aya ya 34 ya *Suratil Tuur* iliyoteremka Makka, "Basi nawalete Hadithi kama hii; ikiwa wanasema kweli". Walipo kuwa hawakuweza kuleta Sura nyingi (na Qurani ni Sura 114) waliambiwa katika Aya ya 13 ya *Surat Hud* iliyoteremka Makka, "Basi leteni Sura kumi za uwongo zilizotungwa mfano wa hii"

Walipokuwa hawakuweza hata kuleta hizo Sura 10 waliambiwa katika Aya ya 38 ya *Surat Yunusi* iliyoteremka Makka "Hebu leteni Sura moja mfano wake". Na wakambiwa katika Aya ya 23 ya *Surattul Baqarah* iliyoteremka Madina, vile vile, "Basi leteni Sura moja iliyofanywa na (mtu) aliyemfano wa huyu".

Kisha katika Aya ya 24 ya hii *Suratil Baqarah* aliwakatisha tamaa ya kuweza kufanya haya akasema: "Na hakika hamtafanya kamwe."

Basi mpaka Mitondogoo wa kiyama hakuna atakaye weza kuleta alau Sura moja mfano wa Sura ya Qur-an.

32. Hawayataki kabisa mambo ya haki na uadilifu na wema aliyokuja nayo Nabii Muhammad (s.a.w.)

37. Ili Mwenyezi Mungu apate kuwapambanua walio wabaya na walio wazuri na kuwaweka wabaya juu ya wabaya wengine na kuwarundika wote pamoja na kuwatupa katika Jahanamu. Hao ndio waliokhasirika.

ليميز الله الخبيث من الطيب ويجعل الخبيث
بعضه على بعض فيركمه جميعا فيجعله
في جهنم ۚ أولئك هم الخاسرون ٣٧

38. Waambie wale waliokufuru: "Kama wataacha (yale mabaya waliyokuwa nayo) watasamehewa yaliyopita, na wakiyarudia (tutawatesa kama tulivyowatesa wao mara zilizopita na kama tulivyoitesa hiyo mijikafiri mikubwa ya zamani); imekwisha kuwapitia mifano ya (mambo yaliyowapata) watu wa zamani."

قل للذين كفروا إن ينتهوا يغفر لهم ما قد
سلف ۚ وإن يعودوا فقد مضت
سنت الأولين ٣٨

39. Na piganeni nao (makafiri) mpaka yasiweko mateso (nyinyi kuteswa na wao kwa ajili ya dini kama wanavyokuteseni sasa); na dini iwe kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (asitaaradhiwe mtu kuabudu dini anayoitaka). Lakini wakiacha, basi hakika Mwenyezi Mungu anayaona wanayoyatenda.

وقاتلوهم حتى لا تكون فتنة ويكون الدين
كله لله ۚ فإن انتهوا فإن الله بما يعملون
بصير ٣٩

40. Na kama wakigeuka basi jueni kwamba Mwenyezi Mungu ndiye Mola wenu, ni Mola Mwema na msaidizi Mwema (atakuhifadhini nao).

وإن تولوا فاعلموا أن الله مولاكم ۚ
نعم المولى ونعم النصير ٤٠

41. Na jueni ya kwamba chochote mnachokiteka (mnachokipata ngawira), basi sehemu yake ya tano ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume na jamaa (zake Mtume) na mayatima na masikini na wasafiri (walioharibikiwa); ikiwa nyinyi mumemuamini Mwenyezi Mungu na tuliyoyateremsha kwa mja wetu siku ya kipambanuzi, siku (inayowafikiana na siku) yalipokutana majeshi mawili (siku ya vita vya Badri—jeshi la Waislamu na jeshi la makafiri). Na Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye uweza juu ya kila kitu.

واعلموا أنما غنمتم من شيء فأن لله خمسه
وللرسول ولذي القربى واليتامى والمساكين و
ابن السبيل إن كنتم آمنتم بالله وما أنزلنا
على عبدنا يوم الفرقان يوم التقى الجمعان ۗ
والله على كل شيء قدير ٤١

---

Wanayakataa katakata; hawayataki tu.

34. Katika mwaka wa 6 wa Al Hijra alitoka Mtume na baadhi ya Masahaba zake kuhiji; Maqureshi wakawazuilia. Wanajiona wao kuwa ndio wenyewe wenye amri ya Makka na hiyo Al Kaaba; kwa kuwa zimo katika mikono yao.

35. Maqureshi na makafiri wenziwao wakifanya ibada zao hapo katika Al Kaaba na kwengineko walikuwa wakipiga kofi kwa mikono yao na kuliza vikorombwe kwa mikono yao na ndimi zao. Basi huku kupiga kofi wakati wa ibada na kutoa sauti za mfano wa vikorombwe si jambo zuri hata kidogo.

36. Hao matajiri wa kikafiri, khasa Maqureshi, walitumia pesa nyingi kufanyia mambo na propaganda za kuuzuilia Uislamu usende mbele. Ikawa kazi yao bure—Uislamu umetawanyika ulimwengu mzima.

Na sasa pia hiyo mibwana mikubwa na midola mikubwa isiyokuwa ya Kiislamu inatumia chungu ya pesa na chungu ya propaganda ili kuuzuilia Uislamu usitapakae. Kumbe huo unatanda tu kidogo kidogo ulimwengu mzima kama alivyokariri kusema Mwenyezi Mungu katika Qurani kuwa Uislamu utatangaa tu hata wakichukia vipi makafiri.